


UKURASA 22

**BENZEMA AMPA VINICIUS BALLON D'OR 2024**

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Julai 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581748
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

UTEKAJI WATOTO

# Wanaharakati wang'aka, wakitaka Polisi iwajibike

UKURASA WA 5

## **Majaliwa** ataka wizara kudumisha ubia sekta binafsi

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitaka wizara na taasisi za serikali kuendelea kupokea maoni ya...

UKURASA WA 5

## **ACT** Wazalendo yalia na ugumu wa maisha kila kukicha nchini

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimezidi kulia na ugumu wa maisha unaowakabili wananchi kutokana na...

UKURASA WA 12&13

## **Simulizi** aliyeahidiwa ajira hoteli ughaibuni, akaangukia ukahaba

USAFIRISHAJI haramu wa binadamu tatizo kubwa la kimataifa ambalo linaendelea kuathiri mamilioni ya...





"Wanaoteka wapo mtaani. Tunasikia watoto wametekwa na wengine wamechinjwa. Hii imeamsha kitu gani kitaifa? Nani amewajibishwa?

**GEMA AKILIMALI**




"Hii taharuki imepanda kwa sababu tayari kuna matukio ya kweli yametokea. Ufuatiliaji wa polisi haukuwa wa weledi ndio maana hofu imezidi.

**DK. HELLEN KIJO-BISIMBA**

UKURASA 3




"Taarifa hizo zimekuwa zikileta taharuki, usumbufu na mshtuko kwa wazazi, walezi na watoto. Tabia hiyo pamoja na kwamba ni kosa la jinai ni ya kulaani na kukemewa kwa nguvu kubwa.

**DCP DAVID MISIME**

KUCHOMA MOTO MKE

## Mshtakiwa agoma kwenda Mirembe

UKURASA 7



RIPOTI MAALUM

# Madhila unyanyapaa kwa watu wenye ualbino kujifungua

• **Walia** shida inaanzia kliniki hadi 'leba'...

*Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **DUBE AFUNGUA AKAUNTI YA MABAO YANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Madhila unyanyapaa wenye ualbino kujifungua

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya Watanzania wenye ualbino wamelalama kunyanyapaliwa wanapokwenda zahanati, vituo vya afya na hospitalini kupata huduma za uzazi.

Tazama mkasa huu unaosimuliwa na Clara Majaliwa (34), mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam ambaye ni miongoni mwa wenye ualbino nchini:

"Siku niliyokwenda katika jengo la kuhudumia wajawazito kuanzia kliniki katika hospitali ya... (anataja jina la hospitali), nilikuwa na shauku kubwa, lakini nilikumbana na unyanyapaa wa hali ya juu ambao sikuutarajia.

"Nilipoingia tu katika lile jengo, kundi kubwa la kinamama wajawazito lilinigeukia, kila mmoja ananiangalia na kunishangaa huku wakinong'onezana na wengine kutikisa vichwa, wakionesha ishara zote za kunionea huruma.

"Nilijisikia vibaya lakini nikajikaza, ikabidi nitembee huku nikiwa nimeinamisha kichwa changu mpaka alipokuwa mtoahuduma za afya ya uzazi ili kuelekezwa utaratibu."

"Muuguzi aliponiona, naye akahamaki na kuniambia maneno yaliyogeuka maumivu makubwa moyoni mwangu.

"Alitamka 'yaani na wewe umebeba mimba? Haujihurumii kwa hali yako ya ualbino? Hivi huwa mnafikiria nini nyie watu? Sasa wakati wa kujifungua itakuwaje?'"

Mama huyo wa watoto watatu ambao hawana ualbino, anasema kauli ya muuguzi ilimfanya aogope na kujutia uamuzi wake wa kubeba ujauzito, hata akahisi yeye kubeba ujauzito ni kukaribisha kifo.

Clara anasema mama yake mzazi alifanya kazi kubwa ya kumweka sawa kisaikolojia ili aendelee na safari yake ya kliniki.

"Mama yangu aliniambia kuwa si kweli kwamba kwa kubeba ujauzito ningekufa kwa sababu alikuwa ameshuhudia wanawake wengi wenye ualbino wakijifungua salama, hivyo akanitaka nisiogope," Clara anasema.

Clara anasema kuwa mwezi uliofuata aliamua kubadili hospitali, alikwenda hospitali nyingine ya serikali kuanza upya kliniki ili kuepuka maneno ya kuudhi yaliyotolewa dhidi yake alipokwenda hospitali ya awali, lakini huko kwenye hospitali ya pili nako mambo yakawa hivyo hivyo.

"Baada ya kukumbana na madhila hayo, niliamua kujikaza, nikaendelea na kliniki katika hospitali hiyo ya pili hadi nilipojifungua.

"Cha ajabu ni kuwa, baada ya kujifungua, manesi waliitana na kuzunguka kitanda changu, wakimshangaa mtoto wangu aliyetoka na rangi nyeusi ilhali mimi nina ualbino.

"Ile siku niliyojifungua nilikuwa kama kivutio cha hospitalini. Kila baada ya dakika chache, nesi mpya anakuja kumwangalia mtoto na kuniuliza maswali ya karaha kama vile 'mume wako ni kama wewe (yaani mwenye ualbino)? Clara anasimulia.

Clara anasema alipitia madhila ya aina hiyo katika miaka minane ya safari yake ya uzazi wa watoto watatu iliyoanza mwaka 2014 hadi 2022.

Mama huyo anaeleza kuwa kama asingekuwa na mshauri wa mama yake mzazi, pia elimu ya darasani (msomi mwenye Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Miradi), asingehudhuria kliniki na angejifungulia nyumbani.

Si Clara tu aliyekumbana na unyanyapaa huo. Asha Boniface, mwenye ualbino, anasema hatosahau siku aliyokwenda kutoa kijiti cha uzazi ili kubeba ujauzito wa mtoto wake wa pili katika moja ya hospitali za serikali mkoani Dar es Salaam.

Asha anadai kuwa nesi aligoma kumpa huduma kwa maelezo kuwa amsubiri nesi mkuu "kwa kuwa ngozi yake ni nyeti sana".

Mama huyo wa watoto wawili anasimulia, "Siku hiyo nilikwenda kwa ajili ya masuala ya uzazi wa mpango, nesi niliyemkuta aliniambia 'suala lako ni tofauti na wengine kwa sababu ngozi yako ni 'sensitive' (nyeti), ngoja mkuu wa kitengo aje kunisaidia kwa sababu sitaki kesi.

"Nilikwenda kusubiri kwenye benchi kwa saa tatu bila msaada wowote mpaka mume wangu alipokuja na kunishauri twende hospitali binafsi."

Patrick Leonard, mkazi wa Dar es Salaam anayejitambulisha kuwa mkewe anayemtaja kwa jina moja la Dorice, ana ualbino, anasema maneno ya manesi anapomsindikiza kliniki mkewe huyo, yanafanya ajisikie vibaya.

Leonard anasema kila wanapohudhuria kliniki, anahisi kuhukumiwa kana kwamba amemwingiza mkewe huyo katika shida.




"Mfano, niliwasikia wakimwuliza mke wangu, 'mtoto amefanana na baba yake? Baba yake rangi gani?' Walikuwa wanauliza tu kinafiki ili kujua rangi ya baba yake. Kama ningekuwa simpendi mke wangu ningeshamkimbia," analalama Leonard.

Mary Kijagwa, mkazi wa Dar es Saalam, pia analalamika kunyanyapaliwa kutokana na kuwa na ualbino alipokwenda hospitalini jijini kupata ushauri wa njia ipi sahihi ya uzazi wa mpango atumie.

"Maneno ya ajabu yalitolewa dhidi yangu. Tulishazoesha akili zetu kuvumilia maneno ya unyanyapaa mitaani kwetu, sikutegemea yatolewe katika vituo vya afya ambako kuna wahudumu wasomi," anasema.

Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) linasema si hao tu waliopitia changamoto hiyo ya kunyanyapaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Utafiti wake uliofanywa kwa kushirikiana na Shirika la Handicap International kuhusu Hali ya Haki za Watu Wenye Ulemavu nchini, ulibaini mambo linayoyaita "ya kushangaza".

Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti huo, katika mikoa 13 ukiwamo wa Dar es Salaam, asilimia 55 ya watu wenye ulemavu walikiri hukumbana na changamoto wanaposaka huduma za afya, wanawake wakiongoza kwa kunyanyapaliwa.

Hali hiyo inakinzana na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 ambayo katika kifungu cha 26(2) inaelekeza kutoa haki kwa kundi hilo kupata huduma za afya bila kubaguliwa au kunyanyaswa.

Vitendo hivyo pia vinakiuka Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inaelekeza kuwa, "Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki bila ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria."

Vilevile, Katiba hiyo, Ibara ya 13(4) inaelekeza kuwa, "ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote ile inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi."

Mweka Hazina wa Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), Abdilah Omary, anathibitisha kuwa na taarifa kuhusu kundi hilo kunyanyapaliwa katika baadhi ya maeneo ya kutolea huduma, hasa kwenye hatua ya uzazi.

Anasema wengi wao wanapokwenda hospitalini, wanachukuliwa katika dhana tofauti kwamba hawakustahili kubeba ujauzito au kutumia njia za uzazi wa mpango kutokana na hali yao ya ngozi.

"Kauli nyingine zinakatisha tamaa kwa watu wenye ualbino, 'mwanamke atajifunguaje ngozi yake laini, atachanika mwili mzima'," Omary anasema akinukuu baadhi ya dhana dhidi ya kundi hilo.

Alisema kuwa hali hiyo inawatia hofu baadhi yao, akionya kuwa ni kauli zinazovunja na kukiuka haki za msingi za binadamu.

Omary anashauri serikali iendelee kutoa elimu dhidi ya mitazamo hasi kwa watu wenye ualbino na isisitize watu kuchangamana bila kubaguana kutokana na maumbile hasa vijijini ambako anadai ndiko watu wanahitaji zaidi elimu hiyo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Maisha ya Amani kwa Watu Wenye Ulemavu, Sofia Mbeyela, anasema malalamiko mengi wanayoyopokea, yanatoka vituo vya kutolea huduma za afya, hasa huduma za uzazi.

"Baadhi ya madaktari na watoahuduma wengine wa afya wana mtazamo hasi kuhusu watu wenye ualbino, lakini nilichogundua wengi wao hawana elimu, na wanafanya kazi hiyo pasi na kuwa na wito au wanapuuzia miongozo ya Wizara ya Afya, hivyo niwaombe tu wabadilike," Amani anasema.

Daktari katika Hospitali ya Magomeni, Patric Boniface, ananyooshea vidole baadhi ya watumishi wenzake wa kada hiyo, akieleza kuwa wapo baadhi ya wauguzi wenye tabia ya kunyanyapaa wagonjwa, akionya kuwa ni vitendo hivyo kinyume cha maadili yao ya kazi.

"Tunapokuwa tunasoma kumhudumia binadamu, tunafundishwa kwa kila aina ya mgonjwa. Mimi nipo tayari kuhudumia mtu wa kundi lolote, inapotokea muuguzi anamnyanyapaa mwenye ulemavu, hiyo inakuwa ni tabia yake binafsi," anasema Dk. Boniface.

Mratibu Huduma za Afya ya Uzazi Mama na Mtoto Mkoa wa Dar es Salaam, Agnes Mgaya, anasema wameweka mfumo wa kupokea malalamiko dhidi ya mienendo ya watoahuduma za afya, ukijumuisha mabango yenye namba za mganga mfawidhi wa kituo na namba ya simu ya huduma kwa wateja inayopokewa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) moja kwa moja.

Hata hivyo, Agnes anasema hajapokea malalamiko rasmi kuhusu mtu mwenye ualbino kunyanyapaliwa na watoahuduma.

"Inapotokea mtu yeyote, bila kujali rangi yake ya ngozi, ananyanyapaliwa, ana haki ya kufikisha malalamiko sehemu husika ili kusaidiwa na hatua stahiki kuchukuliwa dhidi ya aliyemnyanyapaa," anasema Agnes.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, anaungana na TAS kushauri serikali na wadau wa haki za binadamu waendelee kutoa elimu kwa watoahuduma na jamii kuhusu ulemavu.

Dk. Anna pia anashauri kufanyike ufuatiliaji wa vitendo vya unyanyapaa katika vituo vya kutolea huduma za afya na kuwafikisha wahusika katika vyombo vya haki ili wengine waone mfano na kubadilika.

"Sera ya Afya izingatie haki na mahitaji ya kundi hili (watu wenye ulemavu). Tatizo kubwa ni jamii kutokuwa na uelewa kuhusu haki za watu wenye ulemavu, ikiwamo uzazi kwa wanawake wenye ulemavu. Pia kuna utekelezwaji hafifu wa sheria zinazohusu kundi hilo.

"Kisheria mwanamke mwenye ulemavu ana haki kama mwanamke mwingine yeyoye. Tofauti ni kuwa wanawake wenye ulemavu wana changamoto nyingi zaidi," Dk. Anna anasema.

Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, yaliyonesha kuwa Tanzania ina watu wenye ulemavu 2,641,802. Kati yao, wenye ualbino ni 16,477 sawa na asilimia 0.04; Dar es Salaam ikiongoza kwa kuwa na na wenye ualbino 1,637.


**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Madalali tajwa hapo chini kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kwa wadaiwa kulipa madeni yao. Baada ya hapo hatua nyingine za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na uuzwaji wa mali walizoweka dhamana ya mikopo kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Amandus Jovith Hillary | Nyumba Kingázi 'A' Kata ya Kwembe DSM | 16/08/2024 | Eagle Recoveries |
| Yahaya Khalid Ally | Nyumba haijaisha - Kiegea Á' Morogoro | 23/08/2024 | Eagle Recoveries |
| Marry Richard Mwavala/ HP Planner | Nyumba ipo Tabata Kisiwani No. ILA/TBT/TKS33/185 | 15/08/2024 | King Africa General Enterprise |
| William Patrick Chiboni/ Getrude Njau | Gari T.656 DPD Land Cruiser Prado -Tabata yard | 09/08/2024 | King Africa General Enterprise |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**EAGLE: 0767828253/0754684515**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**
**KING AFRICA: 0687956756/0718399636**

HABARI KITAIFA

# Wanaharakati wahadharisha matukio ya watoto kutekwa

**Na Restuta James**

WAKATI hofu ya kuibwa na kuteka watoto ikitanda, wanaharakati wa haki za binadamu wamelitaka Jeshi la Polisi kufanyia kazi taarifa za kupotea, kutoa mrejesho mapema na kuweka bayana matukio hayo.

Vilevile, wamelitaka jeshi hilo kuepuka kukanusha kwa haraka taarifa zinazotolewa badala yake lichunguze na kueleza ukweli ili kuondoa lawama kuwa linatetea na kujiosha linapotuhumiwa.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam juzi, mwanaharakati wa haki za binadamu, Dk. Hellen Kijo-Bisimba, alisema kumekuwa na matukio ya kweli ya kuibwa watoto huku baadhi ya taarifa zikiwa za uzushi.

"Hii taharuki imepanda kwa sababu tayari kuna matukio ya kweli yametokea. Ufuatiliaji wa polisi haukuwa wa weledi ndio maana hofu imezidi.

"Ningeshauri polisi wawe wakweli, waeleze kile kilichotokea na hatua zilizochukuliwa kuliko kusema hakuna hayo matukio wakati yapo," alisema.

Dk. Hellen alishauri watu wanaotoa taarifa za upotoshaji, wakemewe na Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua ili kupunguza uzushi.

"Matukio yakitokea polisi watoe taarifa sahihi, yale ambayo hayajatokea wanaozusha wachukuliwe hatua. Hii itawatoa hofu wazazi.

"Kukanusha tu wakati tumeona mtoto akiwa amewekwa katika kiroba huko Kijichi na tunaona wazazi wakivamia shuleni kudai watoto si sawa. Polisi wachunguze haraka na kuchukua hatua stahiki," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Solidarity for Women and Child with Disability (SOWOC), Adeline Mluge, alisema Jeshi la Polisi limechangia kuongeza hofu kwa madai kuwa limechelewa kutoa taarifa sahihi kwa umma.

"Hakuna mzazi ambaye anaweza kutulia, akisikia kuna watu wanaiba watoto. Wa kuituliza jamii ni Jeshi la Polisi kuhakikishia wananchi kwamba lipo macho na ionekane hivyo kwa kuimarisha ulinzi," alisema.



Alishauri viongozi wa dini kukemea ukatili huo kwa watoto kupitia misikiti na makanisa kwa kuwa ni vitendo vilivyo kinyume cha uumbaji wa Mungu.

"Yote haya yanatokea kwa sababu watu hawana hofu ya Mungu na watu wamepoteza sana imani. Tumrudie Mungu Watanzania," alisema Mluge.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Gema Akilimali, alisema matukio hayo "yamekuwa na kigugumizi". Jamii inapaswa kuwajibika kuanzia ndani ya familia hadi Jeshi la Polisi.

"Wanaoteka wapo mtaani. Tunasikia watoto wametekwa na wengine wamechinjwa. Hii imeamsha kitu gani kitaifa? Nani amewajibishwa? Tumesikia Rais amekemea, lakini ninafikiri angewajibisha watu wa chini yake," alisema.

Alishauri jamii iimarishe ulinzi shirikishi kwa kupitia polisi jamii ili kuongeza nguvu ya ulinzi mchana na usiku badala ya sasa inavyofanyika usiku pekee.

### TEF YAONYA

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari juzi, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alitaka jamii iepuke kusambaza taarifa za uongo na potofu mitandaoni.

"Tabia hii ya kupokea na kusambaza taarifa ambazo hazina uhakika au ukweli, husababisha taharuki, usumbufu na mshtuko kwa wazazi, walezi, watoto na wananchi kwa ujumla.

"TEF inaomba Watanzania kutoa taarifa ambazo wana uhakika nazo ili kuepuka kusababisha taharuki na hofu kubwa," alisema Balile.

Mwenyekiti huyo pia aliomba wananchi wasisambaze taarifa ambazo hawana uhakika nazo kwa kuwa ni kosa la jinai kisheria na si maadili ya uandishi wa habari kuisumbua jamii.

"Tunatoa wito kwa wazazi na walezi kutimiza wajibu wao wa kuwatunza na kuwalinda watoto wao. Polisi nao wakati tunawasihi kuchunguza matukio yanayotajwa, tunawataka waongeze ulinzi katika maeneo mbalimbali nchini ili kuendelea kuaminika kwa wananchi na wajione wako salama," alisema.

Wiki iliyopita, Msemaji wa Jeshi la Polisi, DCP David Misime, alikemea kutolewa taarifa kuhusu watoto kuibwa na kutekwa, akiitaka jamii izipuuze.

Katika taarifa yake kwa umma, DCP Misime alisema mwezi huu kuna watu wametengeneza taarifa za uongo kuwa eneo fulani watoto wa shule fulani wamechinjwa kisha kusambaza katika mitandao ya kijamii.

"Taarifa hizo zimekuwa zikileta taharuki, usumbufu na mshtuko kwa wazazi, walezi na watoto. Tabia hiyo pamoja na kwamba ni kosa la jinai ni ya kulaani na kukemewa kwa nguvu kubwa," alisema DCP Misime.

Alisema kupokea na kusambaza taarifa ambayo haina uhakika ni kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015.


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Viwanda kipaumbele Dira Maendeleo 2050

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema katika maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, imeweka kipaumbele kikubwa kwenye sekta ya viwanda lengo kubwa likiwa kuondoa utegemezi wa kununua bidhaa nyingi nje ya nchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, alisema hayo juzi wakati akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa viwanda.

Mkutano huo ulioandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), pia ulizindua tuzo za Rais za Mzalishaji Bora Viwandani (PMAYA) ambazo hufanyika kila mwaka kwa wenye viwanda.

Prof. Mkumbo alisema wasomi mbalimbali wamesema kwenye maandiko yao kuwa tofauti kubwa baina ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea zinatokana na maendeleo katika sekta ya viwanda. Alisema nchi zilizoendelea kwamba nchi tajiri zina viwanda vingi wakati nchi zinazoendelea hazina viwanda na zinategemea kuagiza bidhaa nje ya nchi.

"Itakuwa vigumu sana kutengeneza Dira ya Taifa bila kuweka viwanda katikati ya dira hiyo kwa sababu hilo ni la msingi na tafiti nyingi zinaonyesha kuwa hatuwezi kuendelea kwa kuendelea kununua bidhaa nje ya nchi. Lazima tuwe na viwanda vingi tuuze nje," alisema.

Alisema katika utafiti ambao umefanywa na serikali katika maandalizi ya dira hiyo uliohusisha watu 7,668 nchi nzima, waliochaguliwa kisayansi walitaka vipaumbele vitano viwapo kwenye dira hiyo.

Waziri Mkumbo alitaja moja ya vipaumbele vilivyotajwa na wananchi hao kuwa ni viwanda na kwamba asilimia 65 ya malighafi zinazotumika viwandani zinatokana na kilimo, hivyo kilimo nacho kitaendelea kuwa kipaumbele kwenye dira hiyo.

Alisema kipaumbele kingine kilichotajwa kwenye utafiti huo ni uwekezaji mkubwa kwenye rasilimali watu kwa kuwa uchumi wa viwanda unahitaji watu walioelimika vyema katika taaluma mbalimbali.

"Lazima dira yetu ituelekeze kuwekeza kwenye elimu na si elimu tu bali elimu iliyo bora," alisema Prof. Mkumbo.

Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodegar Tenga, alisema wadau wa viwanda wamekutana kujadili Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 na kuzungumzia maendeleo ya viwanda kwa ujumla ili kuhakikisha maendeleo ya sekta hiyo hayasahauliki kwenye dira hiyo.

"Tunashukuru Waziri amezungumza kwamba bila viwanda hakuna maendeleo na ametoa mifano ya nchi nyingi zilizoendelea zilivyopiga hatua kwenye viwanda.

"Hakuna nchi duniani hata moja ambayo iliwahi kupiga hatua kubwa kiuchumi bila kuwekeza kwenye viwanda, hivyo lazima tuwe na mikakati madhubuti. Kuna msemo wa Kiswahili kwamba kupanga ni kuchagua, hivyo tuchague kuwekeza kwenye viwanda ili tusonge mbele," alisema.

Aidha, alisema ili viwanda vifanye kazi vizuri lazima serikali iwekeze pia kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara na reli na kwenye rasilimali watu.

"Maono ya nchi ni kujipanga ili tutimize tulichopanga kwa hiyo CTI tunaamini viwanda ni muhimu na ili kupata rasilimali lazima tuwe na kilimo kwa hiyo lazima tuwekeze pia kwenye kilimo.

"Tumefungua masoko mengi upande wa Afrika Mashariki (EAC), kusini mwa jangwa la sahara (SADC) sasa tujipange kuuza bidhaa zetu za viwanda nje ya nchi badala ya sisi kuwa soko la bidhaa za wenzetu," alisema Tenga.

Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, alisema Tanzania inapaswa kuwa na viwezeshaji vinavyofaa kama teknolojia, rasilimali watu na miundombinu.



Rais Dk Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JKCI kujenga kituo cha matibabu Zambia

**Na Frank Monyo**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), inatarajia kujenga kituo cha matibabu ya magonjwa ya moyo Zambia, ikiwa ni hatua na mikakati kuelekea kuwa kitovu bora cha matibabu ya moyo na mishipa Afrika.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari wa Tanzania na China waliotembelea taasisi hiyo katika kuadhimisha miaka 16 tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo.

Dk. Kisenge alisema taasisi hiyo pia ina mpango wa kuanzisha vituo katika nchi za Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Alisema ushirikiano kati ya China na Tanzania umeiwezesha kwa kiasi kikubwa taasisi hiyo kujenga miundombinu, ununuzi wa vifaa, kujenga uwezo kwa hospitali na matibabu kupitia kuongeza wingo wa uelewa katika matibabu ya moyo kwa kubadilishana ujuzi na kufanya taasisi hiyo kupokea wagonjwa kutoka Afrika Mashariki na Kati.

"Ushirikiano wa serikali za China na Tanzania umechangia katika mafanikio. Bado tunahitaji wataalamu kutoka China katika wakati huu ili kuhakikisha lengo letu kuu la kuwa kitovu cha bara la moyo na mishipa linafikiwa," aliongeza.

Alisema JKCI ilijengwa kwa uhusiano mzuri uliokuwapo awali kwa waasisi na zaidi ya Sh. bilioni 16 zilitolewa na serikali ya China. Alisema mwanzoni kulikuwa na vitanda 152 na kwamba hivi sasa kuna vitanda 252, ikiwa ni pamoja na kutoa hela ya vifaa tiba kutibu magonjwa ya moyo.

Alisema JKCI ni taasisi bora na ya kwanza Afrika Mashariki na Kati katika kutoa huduma bora ya upasuaji na tiba ya moyo.

"Taasisi inatibu wagonjwa wengi sana ukilinganisha na taasisi yoyote Afrika Mashariki na Kati kwani tunafanya zaidi ya operesheni 700 kwa mwaka. Hakuna taasisi nyingine Afrika Mashariki na Kati yenye uwezo huo kupasua magonjwa ya moyo zaidi ya wagonjwa 700.

"Pia katika mtambo unaotumia tundu dogo matibabu ya watoto na watu wazima tunatibu zaidi ya wagonjwa 3,000 kwa Afrika Mashiriki na kati," alisema.

Alisema taasisi hiyo pia ina mpango wa kupanua huduma kwa kuanzisha matawi katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Chato, Kanda ya Magharibi na Arusha mjini kwa Kanda ya Kaskazini.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kwa Watoto, Zhao Lijian, alipongeza uhusiano wa nchi hizo mbili na kuongeza kuwa umechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya.

Alisema wakati wa ushirikiano huo, timu ya madaktari ilitoa uzoefu pamoja na kutoa mafunzo kwa kizazi cha madaktari wa ndani jinsi ya kutumia vifaa vipya kutoa huduma bora za afya.

Katika miaka ya hivi karibuni, serikali ya China ilizindua mpango wa ushirikiano wa matibabu kati yake na Afrika, kuruhusu madaktari wengi wa Tanzania kupata mafunzo ya matibabu nchini humo, kutuma timu za matabibu katika nchi za Afrika kufanya uchunguzi wa bure, programu za matibabu, kambi za mafunzo na kuchangia idadi kubwa vifaa vya matibabu kwa watu wa Tanzania.

Kwa sasa, Tanzania ni timu ya 27 ya madaktari wa China yenye watu 11, iliyowasili Dar es Salaam Januari, mwaka huu.

# TCRA yajivunia TEHAMA katika ukuaji uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema uchumi wa Tanzania umekua kwa kasi kubwa katika kipindi cha miaka mitatu kutokana na kukua kwa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika maeneo mengi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCRA ambaye ni Mkurugenzi wa Masuala ya Kisekta, Mhandisi Mwesigwa Felician, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na maofisa wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) waliotembelea ofisi kuu za TCRA, Dar es Salaam, ikiwa ni ziara ya mafunzo kuhusu masuala ya usalama mtandaoni.

Maofisa waliotembelea mamlaka hiyo wanahudhuria mafunzo hayo ni maofisa wanafunzi wa Chuo cha Ulinzi na Intelijensia Tanzania (TDIC) walioko kwenye wiki ya mwisho ya mafunzo ya wiki 10 ya masuala mbalimbali ya kijeshi.

Kati yao walikuwa wakufunzi wanane (8) na maofisa 31, sita wanawake. Alisema TEHAMA imechangia maendeleo ya sekta mbalimbali zikiwamo elimu, afya, ulinzi na uchumi wa nchi.

Aidha, alitoa mifano wa namna TEHAMA ilivyowezeshi kwenye huduma za kifedha na miamala ya simu, matumizi ya pesa mtandao kwa benki, na ukuaji wa uchumi kidijitali.

Takwimu za hali ya mawasiliano robo mwaka ya Aprili-Juni 2024 iliyotolewa na TCRA inaonesha kuwa akaunti za pesa kwa simu ziliongezeka kutoka 25,864,318 mwaka 2019 hadi 52,875,129 mwaka 2023 na kufikia 55,523,067 Juni, mwaka huu.

# ACT yalia ongezeko ugumu wa maisha

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimezidi kulia na ugumu wa maisha unaowakabili wananchi kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa, utitiri wa kodi, tozo, ushuru na mazingira magumu ya kujipatia kipato.

Kilio hicho kilitolewa juzi na viongozi wakuu wa chama hicho walio katika ziara kwenye mikoa tofauti nchini huku wakifanya mikutano ya hadhara.

Akiwa Kondoa Mjini, Kiongozi wa ACT – Wazalendo, Dorothy Semu, alisema kupanda kwa gharama za maisha kumeathiri uwezo wa wananchi kupata mahitaji ya msingi.

"Tunaona mafuta ya petroli na diseli kwa miaka mitatu imepaa sana kutoka wastani wa Sh.2,040 mwaka 2021 hadi kufikia Sh.3,270 kwa Dodoma. Nauli za mabasi zimepanda na mbolea nazo hazikamatiki, ruzuku kwenye mbolea haiwafikii wakulima," alisema.

Semu, alisema suala la gharama kubwa za bidhaa mbalimbali linawaingiza wananchi kwenye umaskini kwa sababu wanashindwa kununua chakula, kugharamikia afya, maji na umeme.

Akiwa Madaba mkoani Ruvuma, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Isihaka Mchinjita, alisema wananchi mkoani humo wanapitia maisha magumu kutokana na kupanda kwa bei ya mbolea tangu mwaka 2021.

"Usambazaji wa mbolea za ruzuku kwa wakulima hauwanufaishi wakulima walio wengi, hivyo kuwafanya wakulima kushindwa kuzalisha na hatimaye kuingia katika umaskini. Tunafahamu kuwa kilio chenu kikubwa ni kuona mnaipata mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu ikiwa na ubora.

Kwa mujibu wa Mchinjita, bei ya mahindi wanayouza wananchi wa mkoa wa Ruvuma ni Sh.370 hadi Sh.400 kwa kilo.

Naye Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, akiwa Busega mkoani Simiyu, alisema kuporomoka kwa bei ya pamba kutoka kuuzwa Sh.2,000 mwaka 2022 hadi Sh.1,060 kwa kilo mwaka jana, kumeongeza maumivu na hali ngumu ya maisha kwa wananchi wa mkoa huo.

Kiongozi mstaafu wa chama hicho na Mbunge wa zamani wa Kigoma Kaskazini, Zitto Kabwe, akiwa mkoani Kigoma alisema kuna mikoa saba nchini ambayo wananchi wanaishi chini ya mstari wa umasikini na hawana uwezo wa kutumia Sh.1,700 kwa siku.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimkabidhi Ripoti ya Mchango wa Sekta Binafsi katika Uchumi wa Nchi kuanzia mwaka 1992 - 2023, Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula, baada ya kuizindua katika maadhimisho ya Wiki ya Sekta Binafsi 2024 na miaka 25 ya taasisi hiyo, Dar es Salaam juzi usiku. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila. **PICHA: JOHN BADI**

# Majaliwa ataka wizara kushirikisha sekta binafsi kuleta mazingira wezeshi

**Na Faustine Feliciane**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitaka wizara na taasisi za serikali kuendelea kupokea maoni ya sekta binafsi na kuyafanyia kazi ili yaingie kwenye maboresho ya sera na sheria za biashara.

Kwa kufanya hivyo, itasaidia kuondoa vikwazo vya urasimu na kuboresha taratibu za usajili na uendeshaji wa biashara nchini kwa kuwezesha upatikanaji wa vibali na leseni kwa haraka zaidi.

Aidha, akizungumza juzi jijini Dar es Salaam katika hafla ya ufunguzi wa Wiki ya Sekta Binafsi nchini na maadhimisho ya Miaka 25 ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Waziri Mkuu alisema wizara zinazohusika na viwanda, biashara na uwekezaji zihakikishe zinabuni mbinu bora za kukuza na kusaidia biashara ndogondogo na za kati ili ziwe na manufaa kwa taifa huku wakishirikiana na sekta binafsi.

"Naagiza kuwe na mazingira mazuri ya upatikanaji wa mikopo nafuu na mafunzo pamoja na ufikiaji wa masoko, ili kusaidia biashara ndogondogo na za kati kukua na kuchangia katika uchumi kwani ni wazi biashara hizi ni sehemu muhimu ya kuimarisha sekta binafsi," alisema Waziri Mkuu.

Akieleza jitihada zilizochukuliwa katika kukuza sekta binafsi na uwekezaji nchini, Waziri Mkuu alisema serikali imeimarisha mazingira ya biashara kwa kufanya marekebisho kwenye sera na sheria za biashara ili kuweza kuondoa vikwazo vinavyowakabili wafanyabiashara na wawekezaji nchini.

"Aidha, hatua hizi zimejumuishwa katika uboreshaji taratibu za usajili wa biashara, kupunguza urasimu na kuongeza uwazi, kutoa fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, nishati, miundombinu, utalii, viwanda na kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji," alisema.

Pia alisema serikali ya awamu ya sita imewekeza katika miundombinu ya usafirishaji, nishati, maji na mawasiliano ambayo ni muhimu kwa shughuli za uwekezaji na biashara ili kuimarisha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, wakati akimkaribisha Waziri Mkuu, alisema mafanikio ya sasa katika sekta ya biashara yanatokana na uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan ya kuasisi falsafa mpya ya kushirikiana na sekta binafsi ikiwamo kuondoa ukiritimba (vikwazo).

Mwenyekiti wa Bodi ya TPSF, Angelina Ngalula, alisema serikali imeendelea kutambua mchango wa sekta binafsi kama injini ya kukuza uchumi wa nchini.

"Kwa pamoja kwa kushirikiana na serikali tunataka kufikia malengo ya dira ya taifa ya maendeleo kufika mwaka 2050," alisema Angelina.

Alisema kuwa wanatamani kuona Tanzania inakuwa kitovu cha biashara na uwekezaji kwa bara la Afrika kutokana na rasilimali ilizonazo.

"Pia, tunatamani kuona biashara nyingi zinarasimishwa ili kuongeza wigo wa walipakodi," alisema.

Aidha, alisema wakati TPSF inaanzishwa, ilikuwa na wanachama 33 lakini sasa imefikisha wanachama zaidi ya 500 ambao wanajumuisha vyama vya wafanyabiashara na kampuni makubwa.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Albert Chalamila, alionya kamata kamata ya watu wanaoegesha magari sehemu mbalimbali zinazoitwa sehemu zisizosahihi (wrong packing).

"Huwezi kukamata 'wrong packing' wakati huna 'right packing' (maegesho sahihi), nimewaita wenzetu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) tuangalie jinsi ya kuliweka sawa hili," alisema Chalamila.

Aidha, alisema wanataka kuandaa mkakati kwa kushirikiana na sekta binafsi kuibadilisha Dar es Salaam kimwonekano kwa kukubaliana kuwa na barabara za kulipia ili kuondokana na tatizo la foleni.

Alisema pamoja na kuwa na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), lakini pembezoni hakuna mandhari mazuri ya kuvutia wawekezaji hivyo ni vyema kushirikiana na sekta binafsi ili kuweza kutapata wawekezaji watakaojenga majengo ya kisasa ya biashara kama hoteli na makazi ya muda mfupi.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wasiowajibika katika majukumu yao wawajibishwe badala ya kukumbushwa

**SERIKALI** kila mwaka imekuwa ikipeleka fedha katika mikoa na wilaya kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile afya, elimu, maji, miundombinu ya barabara na madaraja. Pamoja na miradi hiyo, fedha hizo pia hutolewa kwa ajili ya ujenzi wa masoko na majosho kwa ajili ya mifugo na mazao ya wakulima na wafugaji.

Fedha hizo ambazo hutolewa baada ya kupitishwa bajeti ya serikali na mamlaka za serikali za mitaa, hulengwa mahususi kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi hususani ukosefu wa huduma muhimu katika maeneo wanayoishi.

Katika maeneo mengi, kwa mfano, kilio kikubwa cha wananchi ni ukosefu wa huduma za maji na afya. Kutokana na kilio hicho, serikali hupeleka mabilioni ya shilingi ili kujenga miundombinu na kuboresha huduma ili watu wapate matibabu na vipimo bila kutembelea umbali mrefu na baadhi yao, hasa wanawake na watoto kupoteza maisha au maji kwa kile kinachoelezwa katika kampeni ya kumtua mwanamke ndoo kichwani.

Licha ya serikali kupeleka fedha hizo, miradi mingi imekuwa ikitekelezwa kwa mwendo wa kinyonga, hivyo kusuasua kukamilika au kufanyika kwa viwango hafifu kutokana na baadhi ya watendaji kutokuwa waaminifu kwa kufuja sehemu ya mabilioni hayo. Wakati mwingine, baadhi ya miradi inayotekelezwa haiendani na thamani halisi ya fedha zinazotajwa kutumika katika mradi husika.

Hivi karibuni, mathalani, baada ya Paul Makonda kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, alifanya ziara kwenye wilaya zote za mkoa huo na kubaini madudu katika baadhi ya miradi. Katika Wilaya ya Longido, kwa mfano, Makonda alipokea taarifa ya ujezi wa kituo cha afya ambacho thamani yake ilionekana kuwa tofauti na hali halisi. Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, pia katika baadhi ya ziara zake kwenye mikoa ya Ruvuma na Mara, alishuhudia miradi kadhaa kutekelezwa katika viwango vya chini. Katika Wilaya ya Tunduru, alishuhudia kituo cha afya kimekabidhiwa huku kikiwa katika viwango duni. Miongoni mwa vitu vilivyomshangaza ni kuona milango ikiwa imeanza kuharibika kabla ya kituo kuanza kutumika.

Hiyo ni mifano michache inayoonyesha kuwa kuna madudu mengi katika miradi ya serikali inayotekelezwa kwenye ngazi za halmashauri, mikoa na wilaya ilhali kuna viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia na kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa kulingana na thamani ya fedha zilizotengwa. Kila mara viongozi hao wa ngazi za mikoa na wilaya, wakiwamo wakurugenzi na watendaji katika halmashauri, wamekuwa wakisisitizwa kuhusu umuhimu wa kusimamia miradi ili ikamilike kwa wakati na kwa viwango.


Juzi pia Waziri Mkuu Majaliwa aliwaagiza wakuu wa mikoa kuhakikisha wana taarifa za utekelezaji wa miradi iliyotekelezwa tangu mwaka 2021. Pia aliwataka wajiridhishe kama imekamilika au la na ile ambayo haijakamilika, zijulikane sababu za kutokukamilika.

Kuwapo kwa maagizo hayo mara kwa mara kutoka kwa viongozi wakuu wa serikali, kunaonyesha dhahiri kuwa wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na watendaji kuwa wengi hawajui wajibu wao katika nafasi zao ndiyo maana kuna udhaifu mkubwa katika utendaji wao. Ni wazi kwamba mtu anayetambua wajibu wake, vigumu kukumbushwa mara kwa mara na viongozi wa juu yake kuhusu majukumu yake ya kila siku.

Ni wakati mwafaka sasa viongozi hawa wakakumbushwa mara moja hasa kuhusu kujua wajibu wao badala ya hali ilivyo sasa. Ni vyema wale wanaoshindwa kusimamia utekelezaji wa miradi katika maeneo yao wakachukuliwa hatua zikiwamo za sheria kwa kuwa kushindwa kwao ni ishara ya uzembe na uhujumu wa fedha za umma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Maofisa Afya tujipange na kipindupindu, tusingoje madhara ndio tunakurupuka

Na Yasmine Protace

**UNAPOTAJWA** ugonjwa wa kipindupindu, katika lugha ya mtaani tunatamka 'habari nyingine.' Kwa waliokuwapo zama hizo nchini mwaka 1979, Jiji la Dar es Salaam, lilivamiwa na kipindupindu na kilichotufika, hakifai hata kukumbuka.

Wakiwapo wanafunzi, shule zilifungwa kwa miezi kadhaa, hata baadhi ya wanafunzi hao hawakurejea. Ndio hadithi kama hiyo miaka 11 baadaye, katika kambi moja ya kijeshi mkoani Tanga, afande mmoja siku ya Jumapili akachukua baiskeli kwenda nayo eneo la mjini kwa safari binafsi akivaa kiraia.

Alionekana yu kachangamka anapoondoka, lakini kilichomkuta baadaye kupitia maradhi hayo ya kuharisha na kutapika na kasi ya maambukizi yatokanayo na uchafu, naye hakurudi, baada ya kupatikana habari kuzidiwa na maradhi hayo.

Alipoteza naisha akiwa hospitalini siku hiyo hiyo, hata maziko yake yakawa kiserikali, maana taratibu za sheria ya afya hazikuruhusu kushiriki umma, wakidhibiti maambukizi zaidi.

Hadi tunapoweka nukta katika utangulizi wetu huo, inatoa ushuhuda namna mgonjwa anadhurika kwa kasi na athari kubwa.

Msingi wa shida ya kipindupindu unatajwa sababu kubwa ni kula vyakula vichafu, sambamba na kuishi katika maeneo yenye uchafu.

Mtu anapolazwa katika kituo cha afya na wanapomgundua anakipindupindu wanasema kimetokana na chakula ambacho amekula hakikuwa kizuri, anawahiwa kwanza na kinga inayofafanana na vita vya kipindupindu.

Dawa kukabili maambukizi ya wadudu mwilini, huku maji mengi yanakuwa yamepotea.

Tumeona namna ugonjwa huo unavyoripotiwa kuingia, tunaambiwa hali inayohusishwa na ulaji vyakula visivyo salama, ndio inachangia ugonjwa kumwingia mtu.

Tatizo ni kula vyakula visivyo salama ndio sababu ya mtu kupata ugonjwa huo. Hatua za kuikabili kiserikali, makundi muhimu kijamii kama wafanyabiashara, hupewa elimu ya kuhifadhi vyakula sehemu salama, maji ya kunywa yawe salama na maeneo ya biashara nazo ziwe katika hali ya usafi.

Mbali na wafanyabiashara wanaouza vyakula, pia hata wale wauzaji wa matunda yaliyokatwa, vitafunwa, juisi, hutakiwa vitu vyao kuwa katika hali ya usafi ngazi ya juu. Hiyo ni moja ya namna za kupambana na ugonjwa wa kipindupindu.

Elimu imekuwa ikitolewa kwa jamii jinsi ya kujikinga kwa ugonjwa huo; kuhifadhiwa vyakula vilivyopikwa kwa usafi, kunywa maji yaliyo salama, kunawa mikono na kufanyika usafi wa mazingira yanayotuzunguka.

Ni kipindi kinasikika hata mbiu za mgambo au maofisa afya kuwakamata watu wanaotiririsha maji machafu ovyo pale ugonjwa unapozuka, wanaokiuka sheria wakikabiliwa na hatua za kisheria.

Hiyo ndio pia inawafika wafanyabiashara na wajasiriamali wasiohifadhi vizuri mahitaji yao. Hiyo nguvu inatumika sawasawa kusaidia sana baadhi ya mikoa iliyokuwa na wagonjwa wa kipindupindu, idadi yao kutoongezeka kutokana na kuyafanyia yale waliyotakiwa kuyafanya kupitia wataalamu wa afya.

Niseme tunachokiona, kwa sasa, biashara za vyakula zinazidi kuongezeka vituo vya daladala na pembezoni mwa barabara. Unakuta biashara ya matunda yaliyokatwa hayajafunikwa vitafunwa.

Hapo tena kama ni biashara kwa watoto wa shule, kuna mazingira wapo wanaojazana kuzishika na mikono vitafunwa, kisha wanakula hapohapo, lakini hakuna hata maji ya kunawa. Wapo baadhi ya wafanyabiashara wa matunda na vitafunwa wanahifadhi vitu katika makabati, lakini wengine wanahifadhi katika sinia au beseni na hazijafunikwa.

Pembezoni mwa barabara nako, biashara zikiendelea, kuna mitaro michafu, sasa kwa kufanya biashara ziko wazi afya ya walaji usalama wake uko wapi?

Ushauri wa bure ni kwamba, kunatakiwa kuwapo elimu ya usafi inayotolewa kila mara na watu wa afya kwa wafanyabiashara kutokana na wafanyabiashara kuongezeka katika maeneo ya stendi na pembezoni mwa barabara.

Jamani kinga ni bora kuliko kuisubiri ajali! Ni vyema tusisubiri kipindupindu hadi kinaingia, ndio nguvu kubwa itumike kuwafukuza watu wasifanye biashara katika maeneo hayo na hatua zinazofanana na hizo.

# HABARI KITAIFA

## Moto wateketeza vibanda 10 vya wafanyabiashara

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MOTO ambao chanzo chake hakijajulikana, umeteketeza vibanda 10 kati ya 60 vya wafanyabiashara wadogo kando ya Kituo cha Mabasi Msamvu, Manispaa ya Morogoro.

Mwandishi alifika eneo hilo juzi saa nne usiku na kushuhudia moto huo ukichochewa zaidi na mbao na fito zilizotumika kujenga vibanda hivyo huku askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wakiwa katika harakati za kuuzima.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, wakiwamo Mohamed Ally na Freddy Makungu, walisema moto huo ulianza saa tatu usiku.

"Tulianza jitahada za kuuzima na kutoa taarifa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambao walifika eneo la tukio kusaidia kuudhibiti," alisema Makungu.

Mashuhuda hao pia walidai kilichosababisha moto huo ni jiko la mkaa lililoachwa likiwaka katika moja ya vibanda hivyo. Hii si mara ya kwanza kwa tukio la moto kuripotiwa maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa White House, Kata ya Mafisa, Manispaa ya Morogoro iliko stendi hiyo, Saidi Yasini Daudi, alisema kuwa hadi jana, walikuwa hawajajua hasara iliyosababishwa na moto huo.

Ofisa Operesheni kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Mrakibu Msaidizi, Daniel Myalla alisema wamefanikiwa kuudhibiti moto huo usiku wa kuamkia jana kwa kutumia askari na vijana wa kujitolea.

Alisema walidhibiti moto huo kabla haujaleta madhara kwa binadamu na bidhaa zaidi kwa wafanyabiashara ingawa baadhi ya mali na vibanda vimeteketea.



**Tulianza jitahada za kuuzima na kutoa taarifa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambao walifika eneo la tukio kusaidia kuudhibiti.**



Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Immaculate Semesi (wa tatu kulia), akipokea cheti cha tathmini ya athari ya mazingira (EIA) kutoka kwa Meneja wa Usimamizi wa Matumizi ya Zebaki wa Baraza hilo, Dk. Betrina Igulu, Dar es Salaam jana, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la baraza hilo Geita. Wengine ni wafanyakazi wa NEMC. **PICHA JOSEPH MWENDAPOLE**

KESI KUUA MKE KISHA KUMCHOMA MOTO

# Mshtakiwa akataa kupelekwa Mirembe kupimwa akili

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwonga (38) anayeshtakiwa kumuua mkewe, Naomi Marijani na kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa amekataa mbele ya mahakama kupimwa akili katika Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Afya ya Akili Mirembe, akidai kuwa siku ya tukio alikuwa na akili timamu.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba nne ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwonga ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole, wilayani Kigamboni, alimuua Naomi.

Luwonga alidai hayo jana mbele ya Jaji Elizabeth Mkwizu wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya ombi lililotolewa na Wakili wa Mshtakiwa, Mohamed Majaliwa la kutaka mteja wake akapimwe akili katika hospitali hiyo - Mirembe.

Mshtakiwa huyo alifikia hatua hiyo ya kukataa kwenda kupimwa akili baada ya upande wa mashtaka kusoma ombi la Wakili Majaliwa mbele ya mahakama ndipo akanyoosha mkono wake na kutaka kuzungumza.

Jaji Mkwizu alimpatia nafasi hiyo ambapo Luwonga alidai kuwa yeye hayuko tayari kwenda Mirembe kupimwa akili kwa kuwa ana akili timamu, haumwi wala hajisikii tofauti katika mwili wake.

"Mimi siko tayari kwenda Mirembe, nina akili zangu timamu, labda kama nitalazimishwa nitakwenda, lakini si kwa hiari yangu mwenyewe kwa sababu siumwi wala sijisikii tofauti yoyote," alidai mshtakiwa huyo.

Baada ya mshtakiwa kudai hayo, Jaji Mkwizu alitumia muda wake kumwelewesha na kumpa elimu mshtakiwa kuhusu utaratibu wa kisheria katika suala hilo.

"Mshtakiwa hata kama wakili wako asingeomba wewe kwenda kupimwa, mahakama yenyewe lazima ingejiridhisha kutokana na tukio lililotokea, lazima uende kufanyiwa uchunguzi kwamba siku ya tukio ulikuwa katika hali gani," alisema Jaji Mkwizu.

Jaji huyo pia alimweleza mshtakiwa kuwa mtu yeyote hawezi kujijua kama ana utofauti au hana utofauti kiakili ndiyo maana anatakiwa akapimwe. Pamoja na maelezo hayo, Jaji Mkwizu alitoa amri mshtakiwa kwenda kupimwa Mirembe, huku mshtakiwa huyo akidai kushikilia msimamo wake kwamba yupo timamu, akitaka kesi iendelee kusikilizwa.

Mshtakiwa anasubiri amri ya mahakama itoke ili ioneshe atakaa Mirembe kwa muda gani kisha tarehe ya kesi itatolewa.

Awali mshtakiwa baada ya kumaliza kusomewa maelezo ya mashahidi 28 na vielelezo 14 na upande wa mashtaka, alidai kuwa hakuua kwa makusudi na kwamba hata akinyongwa hadi kufa, ukweli ni huo, ataangamia kimwili, siyo kiroho.

Pia alidai kuwa haogopi kunyongwa wala haogopi adhabu yoyote ile, lakini anataka kama akinyongwa, basi ni anyongwe kwa haki kwamba aliua bila kukusudia, "kwa sababu ni ajali tu ilitokea".

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu (Penal Code), adhabu ya kuua bila kukusudia si kunyongwa.

Luwonga aliendelea kudai kuwa, msingi wa kesi hiyo ni maelezo yake baada ya kuwaambia polisi kwamba yeye ndiye aliyeua na ndiye aliyekuwa anajitumia ujumbe mfupi kutoka simu ya mkewe kwenda simu yake.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



HALI YA VYOMBO VYA HABARI

# Watafiti waichambua, watoa mapendekezo



Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba (wa pili kushoto), Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura (kushoto), Mjumbe wa Bodi ya MCT, Dk. Joyce Bazira (wa pili kulia) na aliyekuwa Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, wakizindua Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari Tanzania. **PICHA: MCT**

**Na Salome Kitomari**

RIPOTI ya Hali ya Vyombo vya Habari ya 2022/2023, imekuja na mapendekezo matano yanayogusa maeneo ya marekebisho ya sheria, kuongeza uraghibishi, kuwa na mijadala ya kitaaluma, vyombo vya habari kuwa na sera ya jinsia na mabadiliko ya sera ya habari na utangazaji itungwe kwa pande zote za Muungano.

Ripoti hiyo iliyozinduliwa mwezi uliopita na Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, ilihusisha upande wa Tanzania Bara na Visiwani, ikihusisha mahojiano na wadau wa sekta ya habari na nyaraka mbalimbali zinazohusika na uhuru wa kujieleza, upatikanaji wa taarifa na uhuru wa vyombo vya habari.

Katika utafiti huo wanapendekeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar, zinapaswa kufanya mabadiliko ya sheria zinazosimamia sekta ya habari kwa ajili ya kutengeneza mazingira wezeshi kwa waandishi wa habari kutekeleza taaluma yao ipasavyo.

Aidha, wadau wa habari na wanaharakati wengine waimarishe uraghibishi kwa kusukuma mabadiliko ya sheria za habari, ikiwamo kutungwa kwa sheria rafiki kwa mazingira ya utendaji wa vyombo hivyo.

Pia, taasisi za kitaaluma za waandishi wa habari zikiongozwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT), waanzishe mjadala na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na vyuo vya uandishi wa habari kwa ajili ya kupata suluhisho la kwanini kunakuwa na wanataaluma 'wasioiva' vyema ambao wengi wameshindwa kuhamisha walichofundishwa kwenye vitendo.

Matokeo ya utafiti kwa Tanzania Bara, yanaonyesha kuwa tangu kuingia madarakani kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Machi 2021, amekuwa na maneno na matendo yaliyoifanya tasnia ya habari kuaminiana na kufanyakazi katika mazingira rafiki yasiyoumiza waandishi wa habari.

"Ingawa maneno na matendo ya Rais Samia ni rafiki kwa waandishi wa habari, lakini bado sera, sheria na kanuni ni zile zile, bado kuna matukio ya waandishi wa habari kukamatwa na kunyanyaswa na mamlaka, kunyimwa taarifa. Tunaona kwa mazingira haya kama sheria zitaendelea kuwa zile zile na kukwaza uandishi wa habari," ilisema sehemu ya ripoti hiyo.

Aidha, ripoti hiyo inabainisha kuwa pamoja na hatua chanya zilizopigwa ikiwamo kufunguliwa magazeti yaliyokuwa yamefungiwa, kukutana na wahariri, na licha ya kauli za matumaini za Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (wakati huo), Nape Nnauye.

Kwa sasa Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 iko katika mapitio huku kukiwa na matumaini chanya kwa wadau kwa kuwa itasaidia kuwa na sheria nzuri.

Kuhusu uwekezaji na umiliki, hakuna uwekezaji mpya kwa kuwa bado umiliki uko mikononi mwa wachache na kuwa na nguvu ya ushawishi huku wakifurahia mazingira wezeshi yaliyowekwa na Rais Samia, kukiwa na tatizo kubwa la uendelevu kwa vyombo vyote vya mtandaoni, magazeti, radio na TV.

"Utafiti unaonyesha kuwa kasi ya ukuaji wa tekonolojia, kubadilika kwa sheria na kanuni, ushindani kwa walaji uliosababishwa na kuwapo kwa mitandao ya kijamii, kubadilika kwa mazingira ya biashara na walaji, uwekezaji mdogo na matangazo kutumika kama mbinu ya kuumiza uandishi wa habari. Tunaona ni muhimu vyombo vya habari vikawa na ubunifu kwa kuwa na vyanzo tofauti vya mapato," inabainisha ripoti hiyo.

Aidha, vyombo vya habari vimekuwa vikipata msaada kutoka kwa wadau mbalimbali huku wengi wakiwa na vipaumbele vyao na mahali wanakoelekeza fedha wanazotoa.

Jingine ni mafunzo kwa waandishi wa habari ilibainika bado haviwapiki waandishi wa habari wakaiva inavyotakiwa kwa kuwa wanapokwenda kwenye vyombo vya habari wanashindwa kuhamisha walichosoma kwenye vitendo, huku wadau wakiomba hatua zaidi kutatua tatizo hilo.

Pia, imebaini kuwa waandishi wa habari hawaandiki kwa kina baadhi ya habari kama sakata la DP World (Mwekezaji katika Mamlaka ya Bandari Tanzania), vyama vya upinzani kama Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), na kuhamishwa kwa wananchi katika Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCA).

Matokeo ya utafiti kwa upande wa Zanzibar, walaji wa habari wanapendelea zaidi habari zilizopo kwenye dijitali huku vyombo vya habari kama magazeti, TV na redio huku vikionyesha kutegemeana jambo ambalo linaonyesha kuwa dijitali sio tishio kwa uendelevu na ukuaji wa vyombo vilivyokuwapo.

Aidha, wadau wanaamini kuwa vyombo vya habari kama magazeti, TV na redio, ni muhimu kwa watu hasa kizazi cha zamani na kwamba ni muhimu vikatafuta kutumia fursa ya ujio wa mitandao ya kijamii.

Pia, ripoti hiyo ilibaini kuwa vyombo vya habari visiwani Zanzibar vinatoa huduma zaidi kuliko biashara kwa kuwa wanashindwa kupata fedha za kutosha kutokana na kukosekana watangazaji wakubwa.

"Mtangazaji mkubwa ni serikali ambao hatangazi kwenye vyombo vya habari binafsi, hali inayosababisha vingi kushindwa kumudu gharama za uendeshaji na hivyo kujiendesha kwa shida," alisema.

Kwa upande wa sera, sheria na kanuni, wadau wanaona kuna ukandamizwaji na nyingine zimepitwa na wakati na zinatakiwa mpya ambazo zitakuwa rafiki kwa utendaji wa vyombo vya habari.

Ripoti hiyo imerejelea kauli ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi ambaye Machi 2022, aliagiza sheria zote za vyombo vya habari kubadilishwa, ili kujenga mazingira salama kwa waandishi wa habari kutekeleza wajibu wao wa kitaaluma.

Aidha, akijibu jambo hilo Machi 2023, Waziri wa Habari Zanzibar, Tabia Mwita Maulid, alisema wako kwenye mchakato wa kutunga Sheria ya Huduma za Habari ambayo imefikia asilimia 80 kwa wakati huo.

"Ingawa hadi wakati tunakamilisha sehemu ya kwanza ya ripoti hii mwaka huu, muswada ulikuwa haujafikishwa Baraza la Wawakilishi licha ya jitihada za uragibishi uliofanywa na wadau ambao umechukua muhongo mmoja," alisema.

Kwa upande wa jinsia na maudhui, ripoti hiyo imebaini kuwa Zanzibar imekuwa kikwazo kwa muda mrefu kwenye sekta ya habari, na kwamba kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na wadau mbalimbali huku waandishi wa habari wanawake wataendelea kuwa kwa wakati mgumu kuvunja mizizi iliyopo.

"Katika mazingira ambayo waandishi wa habari wanawake Zanzibar wametokana na mfumo dume uliopo kwenye visiwa hivyo, kukata mizizi hii ni muhimu sana, waandishi wa habari wanawake wataendelea kuongezeka kwa idadi, lakini kuna ukandamizaji na kuachwa nyuma," alisema.

Kuhusu msaada wa kuendeleza vyombo vya habari, ripoti hiyo imebaini kuwa baadhi ya vyombo vya habari vinapokea msaada wa fedha na rasilimali nyingine kutoka kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi, kwa ajili ya kuendeleza wafanyakazi wao na taasisi zao katika programu za miaka miwili.

"Msaada wa raslimali ni vifaa wa kazi kama laptop, ipads, rekoda, viyoyozi na vifaa vya kurusha matangazo, msaada wa kifedha umesaidia waandishi kupata mafunzo na utafiti licha ya kwamba hakuna matokeo makubwa," inaainisha ripoti hiyo.

Kuhusu dijitali, waandishi wa habari wamekuwa tegemezi kwenye mitandao ya kijamii kujipatia taarifa huku wadau wakitaka kutumika kwa mitandao hiyo kutengeneza maudhui nzuri itakayowezesha kupata fedha kutoka facebook, YouTube na x (zamani Tweeter).



## Walioambukizwa vikope waanza kutibiwa

**Na Allan Isack,** KITETO

WATU zaidi ya 400 waliobainika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa vikope (trakoma) katika Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, wameanza kupatiwa matibabu kupitia mpango maalumu wa kutokomeza ugonjwa huo.

Magonjwa tishio ya macho yanayosababisha upofu; ni vikope (trakoma), mtoto wa jicho (cataract) na presha ya macho.

Akizungumzia ugonjwa huo jana, akiwa katika Zahanati ya Dongo wilayani humo, Daktari wa Macho wa Wilaya hiyo, Enock Awary, alisema baada ya kugundulika kwa maambukizi hayo, serikali imeanzisha mpango huo kwa ajili ya kutokomeza ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Dk. Awary, wagonjwa hao ni kati ya wagonjwa 1,768 wanaokadiriwa kupatiwa tiba kupitia mpango huo.

Alisema utekelezaji wa mpango huo, ulianza mwishoni mwa mwaka 2022 na unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu.

Mpango huo unatekelezwa kwa ushirikiano, kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto na Shirika la Kimataifa Helen Keller.

Ofisa mradi kutoka Helen Keller, Allen Lemilia, alishukuru kwa ushirikiano kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Manyara na Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kiteto kwa kutoa nafasi kwa timu ya madaktari kuweza kufika vijijini na kutoa huduma ya matibabu.

Aliongeza kwa kusema, uchunguzi wa awali unaonesha kuwa katika Mkoa wa Manyara kuna wagonjwa 2,441 wanaohitaji huduma za usawazishaji wa vikope ili wasipate upofu wa kudumu huku Halmashauri ya Kiteto ikiongoza kuwa na wagonjwa wapatao 1,768.

**Utekelezaji wa mpango huo, ulianza mwishoni mwa mwaka 2022 na unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu.**

# Mahakama yaweka 'kiporo' shauri dhidi ya IGP Wambura

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Tanga, imeweka 'kiporo' maombi ya shauri dogo la jinai, lililofunguliwa na Kombo Mbwana dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Camillius Wambura na wenzake.

Kombo, kupitia mawakili wake wawili anaiomba mahakama hiyo iilazimishe mamlaka husika au wanaomshikilia kwa muda mrefu kumfikisha mahakamani na kueleza mashtaka yanayomkabili.

Shauri hilo namba 20240718200000236 lililoko mbele ya Jaji Happyness Ndesamburo, lililotakiwa lianze kusikilizwa jana kabla ya kutolewa amri hiyo limeahirishwa hadi Julai 27 mwaka huu kutokana na Jaji huyo kutokuwapo mahakamani hapo.

Shauri hilo, liliahirishwa hadi Julai 27, mwaka huu na Naibu Msajili wa Mahakama hiyo aliyefahamika kama P. Nyaki.

Aidha, jana Wakili wa Utetezi, Peter Madeleka, akizungumza nje ya mahakama hiyo baada ya shauri hilo kuahirishwa alidai kuwa, mteja wao anataka mahakama iibane mamlaka husika ieleze kwa nini imekuwa ikimshikilia kwa muda wote huo?

Hata hivyo, aliendelea kusema kuwa mteja wao anaiomba mahakama iwalazimishe wahusika kueleza, Kombo ana makosa gani? na wao wanafanya hivyo kwa mamlaka gani?

Kwa mujibu wa Wakili Madeleka, Kombo alikwenda mahakamani hapo kupitia mawakili wake, akafungua maombi ya shauri dogo la jinai akiiomba mahakama iilazimishe mamlaka au watu wanaomshikilia kinyume na sheria impeleke mahakamani.

Alisema: "Wanasema Kombo ana makosa, waje wa mwambie Jaji, sisi tupo tayari kuionesha mahakama kwamba alichofanyiwa Kombo ilikuwa siyo haki na hakikuwa sahihi?

Aliongeza: "Ndio maana tumekuja kumwakilisha mteja wetu ambaye kwa takribani mwezi mmoja hajaonekana kwenye jamii na baadaye tukataarifiwa kuwa Jeshi la Polisi lilimkamata na kumpeleka mahakamani kwa njia ambazo wao mawakili wake hawazijafahamu. Na sasa tunaambiwa amehifadhiwa gerezani."



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (wa tatu kulia) na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Daniel Sillo (wa pili kulia), wakipokewa baada ya kuwasili kwa ajili ya kuzindua mradi wa maji na kufanikisha mchango wa ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Endadoshi, Kata ya Qash, wilayani Babati juzi, ambapo Sendiga alichangia mifuko 100 ya saruji na Sillo mifuko 50 ya saruji. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wafurika Hospitali ya Mount Meru kuchangia damu

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

TAASISI ya WHOISHUSSAIN, imeongoza zoezi la upimaji wa macho na ukusanyaji wa damu kwa wakazi wa Arusha ili kukabiliana na upungufu wa damu salama katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru).

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Omary Chande, alisema Arusha ni miongoni mwa mikoa ambayo katika uchangiaji wake wa damu ni mdogo kutokana na wananchi wachache wanaojitokeza kuchangia damu.

Dk. Chande, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, ameagiza waganga wakuu wa halmashauri zote za mkoa huo kutengeneza mpango wa kukusanya damu kila halmashauri na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Hivyo, aliishukuru taasisi hiyo ambayo hujihusisha na kusaidia jamii katika nyanja mbalimbali ikiwamo kutoa misaada inayogusa jamii kama vile kufanya kambi za matibabu, kuchimba visima kwenye uhaba wa maji na kutoa vyakula kwa wasiojiweza.

Mratibu wa damu salama mkoani Arusha, Warda Kaita alisema mahitaji ya damu salama kwa mwaka katika mkoa huo ni lita 18,851 ambapo kila mwezi ni chupa 1,576.

Aidha, mmoja wa wadau wa maendeleo Ghullam Mukhtar, alitoa rai kwa wananchi kupenda kujitolea kutoa damu ili kuokoa maisha ya wengine huku akiipongeza taasisi hiyo kwa kazi zuri ya kusaidia jamii wanayoifanya.

Kwa upande wake, Mratibu wa WHOISHUSSAIN, Dk. Hamza Sajan alisema katika kutoa damu husaidia kuimarisha mwili kwa mtu anayetoa kwa kutengeneza damu mpya, huzuia magonjwa kama shinikizo la damu pamoja na magonjwa ya moyo.

Kadhalika, alisema zoezi hilo hufanyika mara nne kwa mwaka kwa uratibu wa taasisi hiyo.

Alisema: "WHOISHUSSAIN inaamini katika kusaidia kwani tumefundishwa na mjukuu wa Mtume kutoa msaada kwa wengine. Vilevile, tulivyozawadiwa na Mwenyezi Mungu tunapaswa kutoa kwa wengine kwa manufaa mapana zaidi."

Nao baadhi ya waliojitokeza kujitolea damu walisema utoaji wa damu kwa ajili ya kusaidia wengine ndio zawadi pekee ambayo wamejaliwa na Mungu kuweza kusaidia wahitaji. Hivyo ni furaha kwao kuweza kutoa msaada kwa wengine.

Abdulaaziz Hamisi, alisema kutoa damu hakuna madhara yoyote isipokuwa ni kuimarisha mwili kwa kuepukana na maradhi kama shinikizo la damu, magonjwa ya moyo na faida nyingine kubwa ni kutoa msaada kwa wengine pamoja na kuwa na uhakika wa afya baada ya vipimo.

Vilevile, mmoja wa wachangiaji damu, Juma Mbaringo alisema zawadi pekee anayoiona iliyotoka kwa Mungu ni kutoa damu kwa ajili ya wengine ambapo ni zawadi ya asili huku akisema damu haiuzwi wala kuzalishwa.



# Wafanyabiashara watishia kuhamia Uganda

**Na Restuta Damian,** MISSENYI

WAFANYABIASHARA wa nafaka na bidhaa za viwandani wanaotumia mpaka wa Mutukula unaoitenganisha Tanzania na Uganda wamelalamikia kuwapo kwa utitiri wa tozo na ushuru upande wa Tanzania.

Wamesema hali hiyo inasababisha baadhi yao kuamua kuwekeza mitaji yao katika nchi hiyo jirani.

Walitoa kero hiyo juzi kwa nyakati tofauti katika mpaka uliopo wilayani Missenyi mkoani Kagera na kueleza kuwa, utitiri huo wamekuwa wakikumbana nao zaidi forodhani upande wa Tanzania tofauti na ilivyo katika upande wa Uganda.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Wilbrod Sprian alisema vikwazo hivyo ni chanzo cha kuwafanya kutokuwa na maendeleo wao na nchi kwa ujumla kwani inawakatisha tamaa wale wanaohitaji kufanya biashara na kuamua kwenda kuwekeza Uganda.

Alisema wingi wa tozo unawafanya wafanyabiashara kuchukua mitaji yao kwenda kufungua biashara upande wa pili wa Uganda na kutochangia tena mapato kwenye nchi yao.

Wakala wa forodha mpakani hapo, Linus Mhando alisema ipo haja ya kufanya mabadiliko katika taratibu za ukaguzi kwa kuwa na mawasiliano baina ya nchi hizo mbili kwani taratibu zilizopo kwa sasa zinawalazimu kulipia ushuru na kukaguliwa mara mbilimbili.

Naye Mkuu wa Kituo cha Forodha mpakani hapo, Elpidius Bigilwamungu, alisema wingi wa tozo umesababisha kupungua kwa wafanyabiashara hali iliyokifanya kituo hicho kutokufikia malengo ya ukusanyaji mapato.

Alisema pamoja na hali hiyo pia kituo kutokuwa na mashine ya ukaguzi wa mizigo ni sehemu ya sababu iliyofanya wapate makusanyo ya Sh. bilioni 32 kwa mwaka 2023/24 nyuma ya makadirio yao ya Sh. bilioni 36.3.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Balozi Dk. John Simbachawene akizungumza baada ya kutembelea mpaka huo, aliahidi kufanyia kazi uwepo wa matatizo yanayohusu biashara hasa katika suala la ushuru, tozo na vizuizi ili kuwezesha biashara kustawi eneo hilo.

# T.A.G yamkana mchungaji anayedaiwa kuua na kupora gari

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ASKOFU wa Kanisa la Tanzania Assembles of God (T.A.G), Jimbo la Mwanza Kusini, Isack Gwalalika, amesema kanisa hilo halimtambui wala halihusiki na tuhuma za mauaji zinazomhusu Mchungaji John Masanja.

Mchungaji Masanja anatuhumiwa kumuua Majuto Seif ambaye alitambuliwa kama mchungaji wa kanisa hilo.

Alitoa kauli hiyo juzi katika kanisa la T.A.G lililopo maeneo ya Nyegezi Kona alipozungumza na waandishi wa habari walioitwa kwa ajili ya tamko la kukanushwa kwa hatua ya mtuhumiwa huyo kujitambulisha kama mchungaji wa kanisa hilo. Askofu Gwalalika alisema kanisa hilo liliona taarifa zilizotolewa na Jeshi la Polisi Julai 5 mwaka huu kuwa mtuhumiwa huyo alijitambulisha kuwa ni mchungaji wa Kanisa la T.A.G, ikiwa siyo sahihi hivyo kumtaka mtuhumiwa huyo kutojitambulisha kuwa ni mchungaji wa kanisa hilo.

Hivyo, alilisihi Jeshi la Polisi kujiridhisha kwanza na taarifa zinazotolewa na watuhumiwa kabla ya kuzitoa kwa umma na kuwa baadhi ya watuhumiwa hutoa taarifa za uongo.

Alisema T.A.G lenye washirika 193,741 nchini, likiwa na majimbo matatu mkoani Mwanza, makanisa 131 na washirika zaidi ya 13,000 linatambua weledi wa Jeshi la Polisi, akisema wataendelea kushirikiana nao katika kujenga taifa.

Julai 5, 2024 Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza lilitoa taarifa ya kukamatwa kwa George Masangya (35) Mchungaji wa T.A.G lililopo Kata ya Buhongwa, Wilaya ya Nyamagana ambaye alikamatwa Julai 3, 2024 kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya Majuto Seif (38) mkazi wa Mtaa wa Usagara. Akitoa taarifa hiyo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza DCP Wilibroad Mutafungwa alisema baada ya mauaji hayo mtuhumiwa huyo pamoja na wenzake walipora gari lenye namba T.851 ECU mali ya Bertha Yohana.





Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, akionesha POS Mashine kwa waandishi wa habari, mkoani humo jana, iliyokuwa ikitumiwa na watumishi wanne wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuiibia mapato serikali, ambapo wametiwa mbaroni. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kanda ya Ziwa kinara ukiukwaji haki ya kuishi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MRATIBU wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Ole Ngurumwa, amesema tathmini iliyofanywa na mtandao huo imebaini kuwa, mikoa ya Kanda ya Ziwa inaongoza kwa ukiukwaji wa haki ya kuishi.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Mwanza wakati akizungumza na vyombo vya habari.

Alisema miongoni mwa viashiria vya ukiukwaji huo ni pamoja na vifo vya watu wanaodaiwa kuvamia migodi mkoani Mara, mauaji ya watu wenye ualbino.

Viashiria vingine alisema ni pamoja na matukio ya utekaji na upotevu wa watu akitaja matukio yaliyotokea hivi karibuni mkoani Geita pamoja na Ngara mkoani Kagera. Hivyo kanda hii inaongoza kwa uvunjifu wa haki hiyo kulinganisha na kanda zingine.

Mratibu wa mtandao huo, Kanda ya Ziwa Magharibi, Madage Joseph, alisema kufuatia juhudi za mtandao huo kwa kushirikiana na vyombo vya usalama na utetezi wa haki za binadamu wamefanikiwa kudhibiti vitendo vya unyanyasaji na mauaji mkoani Shinyanga kwa asilimia kubwa.

# OUT yapendekeza maboresho mfumo wa elimu

**Na Halfani Chusi**

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Prof. Elifas Bisanda ameshauri kufanyika kwa mabadiliko katika mfumo wa elimu ili uwe wa kisasa.

Alitoa ushauri huo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa sherehe ya kutimiza miaka 30 tangu chuo hicho kilipoanza kutoa mafunzo nchini.

Prof. Bisanda alisema kitu kibaya ambacho wakoloni walifanya ni kuua mfumo wa elimu ya kujitegemea na kurithisha mfumo wao ambao kila mwaka mwanafunzi anasoma darasa moja.

"Mtu anakaa shuleni miaka 18 akitoka hawezi kufanya chochote, zamani kama baba yako ni mfinyazi anakufundisha kufinyanga ukiolewa baada ya mwezi mmoja wewe ni mfinyanzi na utapata wateja," alisema Prof. Bisanda huku akiahidi kuendelea kuishauri serikali kufanya mabadiliko zaidi katika sekta ya elimu.

Pia alishauri mitaala ya walimu iendane na maudhui yaliyoko katika mitaala mipya ya elimu ambayo imejikita zaidi katika elimu ya mafunzo kwa vitendo.

Aidha, alisema: "Mitaala ya kwenda kwenye hatua ya shahada tumeshauri ibadilishwe iwe ya amali ili wahitimu wawe watu wa kuanzisha fursa za ajira na biashara, siyo kusubiri ajira kwa kuzunguka na kukaa barabarani".

Aliongeza: "Leo tunahangaika lakini bado tunatoa wahitimu wasioweza kufanya chochote. Aidha, serikali ni sikivu na hayo yote tunayozungumza inasikia hivyo mfumo wa elimu ya Tanzania utabadilika na kuwa chanya zaidi.

Akitolea mfano, alisema Nigeria kuna jimbo moja Gavana aliagiza walimu wote wa sekondari wafanye mtihani wa kidato cha nne, matokeo yake walimu 20,000 walifeli akawafukuza kazi akaajiri wengine.

Alisema anauhakika ikifanyika hapa nchini walimu wengi watafeli kwa kuwa hawajiendelezi kwa sababu akishajua yeye ni mwalimu kazi yake ni kufuga kuku, mbuzi na kutembea na kiboko.

# ama
## AFYA NA MAZINGIRA





Ukurasa 12

**USAFIRISHAJI HARAMU BINADAMU**
**Simulizi aliyeahidiwa ajira hoteli ughaibuni, akaangukia ukahaba...mtihani 'kufa kupona'!**



**Chuo Kikuu Dar wabuni 'energy drink' isiyo na kafeini pia ni tiba**

Ukurasa 14

# Siku Rais aliponadi Bima Afya, huku akionya kuoza watoto zao lake 'njiti'

**Na Mwandishi Wetu**



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa katika Hospitali ya Rufani Katavi, mjini Mpanda Julai 14, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO.**

***Alhamisi wiki iliyopita, safu hii iliripoti ziara ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika mradi wa kujengwa Hospitali ya Rufani Katavi, hapo akaacha na salamu. Fuatilia kijichojiri:***

AKIWA ziarani mkoani Katavi, Dk. Samia Suluhu Hassan, akanadi Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote iloyopitishwa hivi karibuni, akitoa wito kwa wakazi wa Katavi na Watanzania wote, kila mmoja kuwa na bima ya afya.

Hapo akafafanua kwamba, ni nyenzo itakayomsaidia kupata matibabu, yeye na familia yake, ili kuepusha usumbufu wakati wa kupatiwa huduma za matibabu kipindi mtu atakapougua.

Ilikuwa Julai 14, wakati akizungumza na watumishi wa afya wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Katavi mjini Mpanda, akiwaambia:

"Niwaombe sana watakapokuja Mfuko wa Bima ya Afya, kila mwananchi anunue bima yake na familia yake. Maana yake, unakata bima yako mara moja kwa mwaka, unatibiwa mwaka mzima.

"Mtusaidie kununua bima ya afya, ili tuweze kujenga na kutoa huduma za afya katika hospitali kama hii na hata hospitali za taifa, kanda, mikoa, wilaya na kata," anasisitiza Rais Dk. Samia.

Akaelekeza wito kwa Watanzania wakate bima ya afya, ili kila Mtanzania afya yake iweze kuimarika, kwa kujiimarisha na uhakika wa matibabu wakati atakapokuwa ameugua.

Anasema serikali imedhamiria kupeleka huduma bora za afya karibu na wananchi, kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika hospitali zote nchini, kuhakikisha vifaa tiba vya kisasa, dawa na vitenganishi, pamoja na miundombinu.

Anasema inakuwa jambo jema kwa wananchi kupata huduma bora katika maeneo yao, akitoa ufafanuzi unaowahusu:

"Hii ni Hospitali ya Rufani ya Mkoa. Lakini, ndani ya mkoa tumefanya kazi kubwa ya kuwekeza idadi kubwa ya vituo vya afya, hospitali za wilaya na vituo vya kata na kule chini kwenye zahanati."

Rais Samia akaeleza masikitiko yake, baada ya kutembelea wodi ya kinamama, alikokuta idadi ya waliojifungua wengi wao ni mabinti wa umri kati ya miaka 14 hadi 19.

Kutokana na hali hiyo, amewaomba wazazi hao kuwapa muda wa kusoma watoto wao, badala ya kuwaozesha na kuzaa katika umri mdogo, kunakochangia kujifungua mabinti hao wakijifungua katika watoto 'njiti'.

Vilevile, akawataka waganga wakuu wa mikoa na watumishi wote wa afya nchini, kutoa huduma bora kwa wananchi kama walivyoapa katika viapo vyao vya taaluma.

**SHERIA YA BIMA**

Msingi wa Sheria ya Bima ya Afya Kwa Wote, inafafanua kwamba imeundwa kwa ajili ya kuweka masharti ya kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wengi kupitia bima ya afya.

Aidha, inatajwa kutoa nafasi ya kuanzisha mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote, kuweka masharti ya kupanua wigo wa huduma mbalimbali za afya na kuweka masharti mengineyo yanayohusiana nayo.

Akitoa ufafanuzi bungeni, Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel, akasema Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, kwenye kikao cha Bunge la 12, kwamba, serikali imeanza maandalizi ya kutumika kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Dk. Mollel akaahidi hatua ya kuanza, kuna uwezekano wa kuteua Kifungu cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, vya kuanza kutumikia.

"Baadhi ya vifungu ambavyo vinaweka mifumo imara ya kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote vimeshaainishwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Sheria itatangazwa...," akatamka Dk. Mollel.

Anasema kuwa, serikali imeshaainisha vyanzo vitakavyohudumia watu wasio na uwezo wakiwamo wajane na watoto wa mitaani.

Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ilipitishwa na Bunge Novemba Mosi mwaka jana na Rais Dk. Samia akaidhinisha na sheria hiyo Novemba 19, mwaka jana na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali Desemba, Mosi.

AFYA



'Wahamiaji haramu' kutoka Afrika, wakiwa safarini kwenda Bara la Ulaya kupitia mitumbwi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

USAFIRISHAJI HARAMU BINADAMU

# Simulizi aliyeahidiwa ajira hoteli ughaibuni, akaangukia ukahaba...mtihani 'kufa kupona'!

**Na Flora Wingia**

USAFIRISHAJI haramu wa binadamu tatizo kubwa la kimataifa ambalo linaendelea kuathiri mamilioni ya watu, licha ya juhudi kubwa za kukabiliana nalo.

Usafirishaji huo kwa ajili ya biashara ya ngono bado ni tatizo katika nchi nyingi ikiwamo Tanzania. Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango mwaka jana katika kongamano la mashauriano la maaskofu, wachungaji na viongozi wakuu Kanisa la

Anglikana akisema: "Tanzania imejitolea kuzuia biashara ya usafirishaji wa binadamu."

Uhalisi wake uko katika simulizi iliyoripotiwa katika televisheni, kwa magumu yaliyomkuta, ikianza na ahadi ya rafiki yake kufanya kazi ughaibuni, kumbe alikuwa ananadiwa kujiunga na biashara ya ukahaba.

Aliyempeleka alimwambia huko yupo shangazi yake atakayemsaidia na asihofu, lakini alipofika huko akapelekwa kwenye nyumba moja ghorofani aliko mwenyeji huyo, aliyejitambulisha kuwa ndiye shangazi nwenyeji wake.

Mgeni alikaa hapo pasipo kupelekwa kokote, hata alipouliza kazini hotelini, akaambiwa subiri. Hapo nyumbani walikuwapo wasichana wanne waliokuwa wakitoka jioni, wanarejea asubuhi.

**KAZI HOTELINI**

Mwenyeji wake akamwambia binti huyo awasikilize wenzake watakalomwambia, huku akianikwa" hakuna kazi ya hotelini, bali ni kazi ya kwenda kutafuta hela kwenye nyumba za ukahaba (madanguro)."

Binti akamwambia hajawahi kufanya mambo hayo, akataka mbadala wa kurudi nyumbani Tanzania.

Akamtaka ampatie pasipoti yake na simu amuandalie usafiri kurudi, kumbe ilikuwa mbinu ya kumkatia mawasiliano na nyumbani kwao.

Baada ya hapo, akamwelekeza afuate maelekezo ya kwenda na wenzake kwenye madanguro na kurudi pale nyumbani.

Bado akaendelea kukataa. Hata akaachwa nyumbani bila chakula huku milango imefungwa, wanaporudi wanamuuliza "bado hujakubaliana na utaratibu huo wa ukahaba?"

Akawa anakataa. Siku iliyofuata wakamletea chakula, kilichotiwa dawa za kulevya, pasipo kujua akiwa na njaa, akala, ghafla akapatwa na usingizi mzito.

Kumbe waliandaliwa wanaume wawili waliofika nyumbani kumfanyia tendo la ngono na wakati kitendo hicho kikifanyika, wenyeji walikuwa wakichukua picha za video.

Alipozinduka akajikuta ana maumivu makali na ndipo akaanza kuonyeshwa zile picha, huku akitishiwa kama hataambatana na wenzake kwenda kwenye biashara, basi picha hizo zitarushwa mitandano aonekane kila mahali. Binti huyo alilia sana. Fuatilia mazungumzo:

**MWANDISHI:** Kwa hiyo wakakuonyesha picha vile ulivyofanyiwa ukiwa hujitambui baada ya kuletewa genge la uhalifu?

**BINTI:** Ndiyo. Basi nikawa nalia pale

wakaniambia sisi siyo mama yako wala shangazi yako. Kinachotakiwa hapa ukubaliane nasi.

Nikawaambia, basi nimekubali nawaombeni mfute hizo picha. Wakaniambia siyo kufuta tu, tutaziweka mitandaoni. Nikapiga saluti, nikaomba msamaha.

Wakasema, umekubali? Nikawaambia ndionimekubali nitafanya.

**MWANDISHI:** Waliokufanyia kitendo hicho walikuwa zaidi ya mwanaume mmoja?

**BINTI:** Walikuwa wanaume wawili

walioletwa pale pale ndani nilipokuwanaishi. Basi, nikawaomba msamaha. Nikawaambia nitafanya. Wakaniambia yaani ulitaka hadi tutumie nguvu? Nikawaambia nimeelewa!



Mwanamke mkulima wa Kiafrika, akiendelea na jukumu lake nchini Nambia.

Nikawaambia ili mimi nifanye, naombeni simu nifute hizo picha kwa mkono wangu.

Wakaniambia haina shida mpaka ukubali kwanza, uende tujue kweli kwamba umekubali. Kwa sababu tayari wale nilikuwa nimeshaelewa akili zao nikasema nitakwenda.

Basi hiyo siku wakanibeba kunipeleka kwenye madanguro. Lakini, pamoja na kwenda nikawa namuomba sana Mungu.

'Nikamwambia Mungu naomba usiruhusu mtu yeyote au mwanaume yeyote anifuate.'

Na kweli ndivyo ilivyotokea. Nikarudi nyumbani wakasema, kweli leo umekubali.

Nikawaambia naomba basi nifute hizo picha, nitakuwa naenda bila ubishi. Basi wakanipa simu zao nikafuta! Baada ya kufuta, sasa tukawa tunaondoka wote.

Kwa sababu sikai na funguo wala kadi za milango. Ili mlango ufunguke, lazima kadi.

Hivyo hunibeba tunaenda wakati wa kurudi, tunarudi wote.

Basi tukienda huko kwenye madanguro naenda kujificha, wakinikosa wananipigia simu, uko wapi? Nakimbia haraka haraka nawaambia nipo sehemu fulani na wakija pale wananikuta.

**NATAFUTA MSAADA:**

Wananiuliza vipi? Bado, nawaambia bado. Wananiambia changamka, zunguka huku.

Nazunguka nao hivyo hivyo. Baadaye nikaanza kutafuta msaada. Simu yangu alipoichukua walifuta hadi namba zangu za mawasiliano. Zikabaki zile meseji za kawaida ambazo nimechat na watu wa kawaida.

Yupo kaka mmoja ambaye ni rafiki yangu sana hapa Tanzania. Nikaja kutafuta namba yake nikaipata. Kumbuka huwezi kuongea mbele yao. Ilibidi hapo nichukue simu yangu niifiche nikaingia chooni ambako lipo bafu kubwa. Nikafungulia maji na kumpigia yule kaka simu.

Nikamweleza, nikamwambia, kaka yangu nina changamoto moja mbili tatu.

Akaniambia wewe nimeshakutafuta sana sikupati. Nikamwambia ni kweli, nikamwelezea yote. Akaniuliza uko wapi?

Nikamwambia hata mazingira niliyopo, ili niweze kuongea kwa mazingira nilipo nimejifungia chooni. Nikamwambia hebu nikupigie 'video call' kama kweli upo chooni akanipigia nikamwonyesha. Akaniambia nitakutafuta baadaye nikusaidie.

Namshukuru Mwenyezi Mungu, baada ya siku mbili akawa amenirejea tena.

**NATISHIWA NIJIRUSHE DIRISHANI:**

Katika zile siku mbili, nikawa nimegoma tena kwenda. Nikawa sikubali. Walikuja takribani wadada 40 wakaniambia sasa wewe utachangua mawili; ujirushe mwenyewe dirishani au tukupige.

Nikawauliza kwa nini mnipige? Na kwa nini nijirushe? Wewe unakaidi, kwanza tunakudai pesa nyingi sana. Nikawaambia niliomba nitafutiwe kazi yoyote tofauti na hii ambayo ninaweza kufanya nikawalipa pesa zenu halafu mimi nikabaki kuwa huru.

Wakaniambia huku hakuna kazi nyingine tofauti na hii, hivyo lazima uifanye.

Wakaanza kunishambulia, wakanipiga wakaondoka wameniacha mle ndani.

Nilikaa wiki nzima nina maumivu makali.

**NILIVYOKULA MAKOMBO YA CHAKULA:**

Muda huo, nakula chakula cha makombo (hapa akalia). Wakimaliza kula ndio wananitengea hayo makombo wakiniambia ni ili niendelee kujifikiria. Siku sita nikawa nakula. Wiki ilivyoisha wakaniambia bado hujafanya uamuzi?

Nikawaambia nihurumieni siwezi, sijawahi kufanya na sitegemei. Wakasisitiza itabidi ufanye umeshafika katika nchi ya watu utaishije na nani atakulisha! Haya, hutaki kufanya, utarudije kwenu? Fanya upate nauli urudi kwenu. Nikawaambia hapana.

Nikaendelea kumtafuta yule kaka rafiki yangu, mtandao huku Tanzania ukawa haupatikani ni kama vile hajaingia online. Ikawa kama vile ndoto yangu ya kupata msaada imepotea.

**UAMUZI WA KUJIRUSHA AFE:**

Nikachukua simu yangu nikawa nimeandaa meseji nikasema hapa nilipo sina uwezekano wa kupata nauli kurudi Tanzania, wazazi wangu wenyewe ni masikini. Nikawa nimechukua uamuzi wa kujirusha nife (akaangua kilio).

Nilijiona nimefika mwisho, sina mtu wa kunisaidia. Siku ambayo niliamua kufanya uamuzi, usiku, nahisi huku Tanzania ilikuwa ni mchana. Yule kaka alinitafuta akaniambia Rukia Shekauti (siyo jina halisi), kuna mtu atakupigia simu atakuelekeza.

Hivyo, fuata maelekezo yake atakusaidia utarudi nyumbani. Hapo ndipo nilipoanza kuona kumbe lipo tumaini kwani nilikuwa nimeshakata tamaa.

Akaniambia usifanye kitu chochote wala kufikiria kitu chochote.

Nilikuwa sipo na nilipokuwa mtandao ulikuwa haupo ndio maana ulikuwa hunipati.

Nikamwambia sawa. Kweli haikuchukua muda, yule mtu kweli akanitafuta. Akajitambulisha akaniambia ndio mimi.

Akaniuliza upo karibu na wapi

nikamwelekeza mahali nilipokuwa naishi. Akaniambia, basi sawa.

Akaniambia shuka chini. Nikamwambia siwezi kushuka chini kwani sina funguo wala sina kadi. Naishi kwa kufungiwa ndani.

Akaniambia sasa usilie jikaze. Muda huu ni muda wa kufikiria wewe ufanyeje ili uweze kutoroka. Maana siyo kuondoka bali kutoroka!

Nikamwambia sawa. Ikabidi sasa nianze tena kuwa mtumwa, niwe ndio wa kupika.

Uchafu tulikuwa tunaweka nje. Unafungua mlango kidogo unaweka nje na kwenye hilo jengo wapo wafanyakazi wanapitia.

Kwa hiyo nikaanza kuwabembeleza nakwenda kumwaga uchafu. Nikaanza kutengeneze mazingira yangu kuwaomba waanze kunituma kwenda supermarket kununua vitu nipate mwanya wa kuondoka.

Mmoja wa wadada akasema huyo asiwe anatoka nje. Mwingine akasema mwacheni tu aende nje atakwenda wapi wakati hana pasipoti, mji wenyewe haujui, hawezi hata kupanda gari. Mwacheni tu awe anaenda.

Basi kila ninapoenda kumwaga uchafu nilikuwa nakariri jinsi ya kutoroka. Siku moja nakwenda kumwaga uchafu, kwenye hicho chumba, pembeni ipo lifti ambayo ni kwa ajili ya kushusha uchafu. Nikashuka nayo nikaona kumbe chini ni kule huwa tunapita kwenda barabarani.

**NATOROKA KWA LIFTI**

Ile lifti ya taka huwa haitumii kadi. Nikaingia tena kwenye ile lifti nikafika tena kwenye kile chumba cha kuishi. Nikajua kuwa kumbe naweza kutoroka kupitia ile lifti.

Nikampigia tena yule mtu aliyenitafuta nikamwambia nimeshapata namna ya kuweza kutoroka. Akasema weka mazingira kisha nijulishe nami sitalala hadi nihakikishe upo mikononi mwangu.

Siku ya kwanza nikashindwa, siku ya pili na ya tatu nakumbuka walirudi asubuhi. Kila wakiondoka wananifungia. Walivyorudi wakasema tuna njaa. Wakaanza kuzozana wenyewe kwa wenyewe kuwa mimi sili, mimi sipiki. Nikawaambia nitawapikia. Shika hela nenda supermarket ukaleta vitu.

Nikashuka wakanifuata nyuma. Nikarudi nikasema jinsi nilivyovaa watashtuka. Acha nivae nguo la kulalia nikavua suruali na tisheti nikavaa nguo ya kulalia.

Nikaendelea kupika wakawa wanaendelea kuvuta 'shisha' na kunywa pombe. Baadaye wakawa wamechoka wamelala. Wengine wakapanda juu kulala wengine wakabaki pale sebuleni wamelala.

Nikaanza kutikisa mmoja mmoja, kila ninayemgusa anasema niache nimechoka. Nikaenda kule juu nikaiba ile kadi ya mlango nikachukua na funguo. Niliporudi nikawaongezea 'A/C' (kiyoyozi).

Ilivyokuwa kali, mmoja akaniita Rukia tuwekee mablanketi nami nikawaletea. Nikajua tayari usingizi umekolea. Kabla ya kutoroka nikaingia chooni nikampigia yule mtu kumwambia hapa wamelala na leo ndio Mungu amenisaidia naweza kuondoka.

Akaniambia hivi nakutumia gari linakufuata hapa ulipo nakutumia picha ya gari na namba zake kwenye 'whatsApp'. Akaniambia usitoke nje mpaka nikupigie simu kwani hiyo gari ikifika yeye kule ataiona.

Ilipofika akanipigia simu gari ipo chini. Ile lifti wanapita wengi na walishajua kuwa huyu dada anaishi kwa fulani. Hivyo, nikatoka vile vile na nguo yangu ya kulalia mtu asinishtukie kwamba natoroka. Ndivyo nilivyoondoka!

Nikafika nikapanda kwenye gari nikapelekwa mpaka kwa huyo mtu akanipokea na nashukuru huyo mtu alikuwa ni mtu wa serikali ya Tanzania.

Baada ya kufika pale nikawa nimemwelezea nilivyokuwa nalishwa makombo na kupigwa. Akanitafutia sehemu akanihifadhi ili afanye mawasiliano na ndugu zangu.

Na kwamba kupitia yeye, pia watu wengine wa serikali, watanisaidia niweze kurudi nyumbani. Baada ya hifadhi nikaweza kuwasiliana na familia yangu kupitia yule mtu wa serikali na kuwaeleza kilichonipata.

Akapambana kunitafutia msaada katika mashirika hadi mimi kuweza kurudi nyumbani. Kurudi Tanzania nilishikwa mkono kwa asilimia 75 na mkono wa serikali na shirika ambalo lilinisaidia hadi kuifikia tena familia yangu.

**MWANDISHi:** Kwanza nakupa hongera naujasiri, uvumilivu hadi kufika nyumbani. Pili, pole kwa yote yasikuvunje nguvu yasikukatishe tamaa, madamu umerudi wewe songa mbele!

Mazingira haya ya kazi wanaweza wakajikuta wanatumikishwa kijeshi huko kwa ahadi labda wakishika uongozi, watapewa nafasi.

Wengine husafirishwa nje, wanajikuta wanatumikishwa katika kazi mbalimbali. Wengine hupelekwa kwenda kuchukuliwa baadhi ya viungo vyao vya mwili, mfano figo ambazo ni tatizo kubwa duniani na zinauzwa kwa pesa nyingi sana.

AFYA

# Chuo Kikuu Dar wabuni 'energy drink' isiyo na kafeini pia ni tiba

**Na Beatrice Philemon**

KATIKA jamii ya leo yenye shughuli nyingi, watu wamekuwa wakitafuta njia mbalimbali za kuboresha nguvu zao na kuongeza utendaji wao wa kazi kwa kutumia vinywaji vya kuongeza nguvu mwilini yaani (Energy Drinks).

Hiyo inatokea bila kufahamu ni vinywaji vya kuongeza nguvu (energy drinks) zenye 'caffein' zinaleta madhara kama vile wasiwasi, kukosa usingizi, shinikizo kubwa la damu, mirija ya damu kuziba, uraibu na matatizo ya mmeng'enyo wa chakula.

Kutokana na madhara hayo kusababishwa na kafeini, Idara ya Sayansi ya Chakula na Teknolojia katika Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) imetengeneza kinywaji cha kuongeza nguvu (energy drink).

Hicho ni kisichotumia vichochezi vya 'Caffein' ili kusaidia Watanzania kuepuka maradhi ya moyo yasababishwayo na matumizi yake kwenye vinywaji vyenye kuongeza nguvu.

Kinywaji hicho kimetengenezwa kwa kutumia matunda asilia yenye virutubisho mbalimbali kama vile madini ya chuma ambavyo damu, Vitamini B9', vinavyozuia ambayo huzuia watoto kuzaliwa na mgongo wazi, madini ya Potassium, Manganese na Amino Acid.

Katika utengenezaji kinywaji hicho, wameongeza matumizi ya vinywaji vya kuongeza nguvu kwa kina mama wajawazito na watoto kwa kutumia matunda mbalimbali ya asilia.

Akizungumza na Nipashe, Masunga Maganga, mwanafunzi kutoka Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anasema kabla ya kutengeneza kinywaji hiki, alifanya utafiti kwa muda wa miezi nane juu ya vichochezi vingine vinavyopatikana kwenye matunda asilia yanayolimwa hapa nchini.

Baada ya hapo, akagundua kuwa vichochezi vinavyopatikana kwenye matunda mbalimbali asilia, ikiwamo 'maca, beet root' yanayolimwa nchini yana uwezo wa kuupa mwili nguvu bila kuleta maradhi ya moyo.

Anasema kinywaji hiki kilichotengenezwa kwa mchanganyiko wa maca na 'beetroot' kinachoitwa 'beet-maca energy drink', akitaja mfano bora wa kinywaji cha kuongeza nguvu mwilini kisicho na kafeini kinachoweza kutoa faida mbalimbali za kiafya.

Pia, utafiti huo umechochewa na tarifa iliyotolewa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete mwaka jana mwezi wa pili kuhusu maradhi ya moyo hasa mishipa ya damu kuziba kutokana na matumizi ya vinjwaji vya kuongeza nguvu mwilini vyenye 'caffein'.

Baada ya kijana aliyepata madhara ya mishipa ya damu inayoelekea kwenye moyo kuziba hali ambayo kitaalamu inayoitwa (Myocardial Infarction) baada ya kunywa vinywaji vya kuongeza nguvu (energy drinks) vyenye vichochezi vya 'caffein.'

Pia, viwanda vingi vinavyozalisha vinywaji vya kuongeza nguvu mwilini (energy drinks) hutumia 'caffein' kama kichochezi kwa sababu utafiti mdogo uliofanyika juu ya aina nyingine ya vichochezi.

Anasema, kinywaji hiki ni kwa ajili ya watu wote ikiwamo wajawazito na watoto kwa sababu hakina 'caffein' na kwa wananchi au wafanyabiashara ambao wapo tayari kupata kinywaji hiki wanaweza kutembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya chakula kwa ajili ya manunuzi.



Masunga Maganga, mwanafunzi wa Shahada ya Sayansi ya Chakula na Teknolojia, Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akifafanua kuhusu kinywaji kipya kisicho na caffein katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (DITF) 'Sabasaba' , Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

### FAIDA ZAKE

Kinatajwa na wabunifu kuwa ni kinywaji cha kuongeza nguvu kisicho na kafeini kilichotokana na mchanganyiko wa 'maca na beetroot, ikitajwa chaguo bora kwa watu wanaotafuta njia ya asili na yenye afya ya kuboresha nguvu katika utendaji kazi wao.

Pia, ni chanzo bora cha virutubisho na ina faida mbalimbali za kiafya ikiwa unatafuta njia ya kuongeza viwango vyako vya nguvu/ nishati bila madhara mabaya ya kafeini, kinywaji cha nishati.

Vinywaji hivyo vinatajwa kuongeza madini ya chuma kwa wingi wa damu mwilini na hivyo kuifanya kuwa na umuhimu mkubwa kwa wajawazito ambao hupoteza damu nyingi wakati wa kujifungua.

Pia husaidia kuepuka maradhi ya moyo, kuongeza matumizi ya vinywaji hivi kwa mama wajawazito na watoto kwa sababu yana madini ya chuma, kuongeza matumizi ya vinywaji vya kuongeza nguvu kwa watu wenye shida na caffein.

### MAANA YA MACA

Maca inatajwa ni mmea wa Andes unaotumiwa kwa karne nyingi kuboresha afya ya uzazi, kuongeza viwango vya nishati, na kupunguza mfadhaiko. Inayo kiwango cha juu cha virutubisho, ikiwa ni pamoja na vitamini B, madini, na asidi ya amino. Maca pia ina misombo (ingredients) inayoitwa macamides, ambayo inaongeza viwango vya nishati na kuboresha hisia.

### FAIDA BEET ROOT

Beetroot ni mboga yenye virutubisho vingi yenye faida nyingi za kiafya. Ni chanzo bora cha nitrati, ambayo mwili hubadilisha kuwa nitriki oksidi, molekuli inayopanua mishipa ya damu na kuboresha mtiririko wa damu.

Hiyo inaweza kusababisha kuboresha utendaji wa riadha, kupunguza shinikizo la damu, na kuboresha afya ya moyo. Beetroot pia ni chanzo kizuri cha vitamini na madini, ikiwa ni pamoja na chuma, potasiamu, na vitamini C.

"Mtu anayetumia kinywaji hiki ataweza kuboresha mtiririko wa damu na utendaji wa riadha na kuongezeka kwa viwango vya nishati," anasema.

Mbali na hilo kinywaji hiki kinaongeza nguvu na kupunguza uchovu. Hii ni kwa sababu matunda ya asili yaliyowekwa yana misombo (ingredients) ambayo inaaminika kuongeza uzalishaji wa nguvu kwenye seli.

Pia matunda yaliyowekwa kwenye kinywaji hiki yanauwezo wa kuboresha hisia na kupunguza dalili za mfadhaiko na wasiwasi. Hii ni kwa sababu matunda hayo yana athari chanya kwenye mfumo wa neva.

Kuboresha utendaji wa riadha: Beetroot inaweza kuboresha utendaji wa riadha kwa kuongeza mtiririko wa damu na usafirishaji wa oksijeni kwenye misuli. Hii ni kwa sababu beetroot ni chanzo bora cha nitrati, ambayo mwili hubadilisha kuwa nitriki oksidi.

### KUPUNGUZA SHINIKIZO

Beetroot pia inatajwa kuweza kupunguza shinikizo la damu, kwa kupanua mishipa ya damu. Hiyo ni kwa sababu ya nitrati katika beetroot, ambayo hubadilishwa kuwa nitriki oksidi.

Aidha inaboresha afya ya moyo, kwamba 'Beetroot', ni chanzo kizuri cha vitamini na madini, ikiwa ni pamoja na chuma, potasiamu, na Vitamini C. Virutubisho hivi vinaweza kusaidia kuboresha afya ya moyo kwa kupunguza cholesterol na kuzuia magonjwa ya moyo.

Kinywaji cha nishati kisicho na kafeini kilichotokana na mchanganyiko wa matunda mbalimbali ikiwamo beetroot na maca ni chaguo bora kwa watu wanaotafuta njia ya asili na yenye afya ya kuboresha nishati na utendaji wao.

Ni chanzo bora cha virutubisho na ina faida mbalimbali za kiafya. Ikiwa unatafuta njia ya kuongeza viwango vyako vya nishati bila madhara mabaya ya kafeini, kinywaji cha nishati.

Vilevile vinywaji hivi vinaongeza madini ya chuma ambayo yanaongeza wingi wa damu mwilini na hivyo kuifanya kuwa na umuhimu mkubwa kwa wajawazito ambao hupoteza damu nyingi wakati wa kujifungua.

Mtuhumiwa wa mauaji, akiwa chini ya ulinzi.



## CMA yaanzisha mfumo dijitali kuondoa migogoro

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mary Maganga, amesema mfumo mpya wa kusajili migogoro kwa njia ya mtandao uliondaliwa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), utaepusha malalamiko na ucheleweshwaji wa haki pamoja na kuongeza ufanisi kwa watumishi wake.

Maganga aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati akifungua mafunzo maalum kuhusu mfumo huo kwa watumishi wa ofisi ya CMA kutoka mikoa mbalimbali na kuwapongeza kwa ubunifu huo.

Maganga alisema: "Mara nyingi tukiwa tunataka kuongeza ufanisi pakwenda ni kwenye mifumo kwa sababu mifumo tunaweza kuitumia popote pale tulipo na bila kuhitaji kwenda kwa uhalisia. Kwa hiyo tuna imani kubwa itaenda kuongeza ufanisi wa tume yetu".

Pia alisema majukumu waliyopewa watumishi hao ni kusimamia haki katika ajira na kuhakikisha wanatatua migogoro kwa njia ya usuluhishi bora ili kufikia asilimia 81 licha ya sasa kuwa asilimia 76.

"Hivyo ingekuwa ni shuleni wanapewa alama ingekuwa ni A au B wamepata. Hivyo, wataendeleza vyema kutelekeza mpango mkakati wao waliyojiwekea," alisema.

Mkurugenzi wa CMA, Usekelege Mpulla, alisema mfumo huo ukianza kutumika utatekeleza lengo la tume kufikia wadau wao ambao ni waajiri na waajiriwa popote walipo kwani wapo kila mahali lakini ofisi zao hazipo kila pa hala.

"Kwa msingi huo tunatarajia kutumia mfumo huo ili tuweze kuwafikia na kuweza kusajili migogoro yao kwa kutumia kompyuta, simu janja na sisi tuweze kuzishughulikia kwa haraka kwani hili ni takwa na ombi la muda mrefu la wadau wetu hasa wawekezaji kutaka huduma za tume ziende kwa haraka," alisema.

# Kamati ya bajeti yasisitiza umuhimu wa takwimu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imesema matumizi ya takwimu ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

**Takwimu sahihi ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla hivyo ni muhimu kuendelea kuzitumia kwa maslahi mapana ya taifa.**

Aidha, imewapongeza Rais Samia Suluhu Hassan na Dk.Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa wanazozifanya katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mwanaasha Khamisi Juma alibainisha hayo juzi jijini hapa, wakati wa ziara ya mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Kamati hiyo pamoja na watendaji kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar.

Alisema: "Takwimu sahihi ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla hivyo ni muhimu kuendelea kuzitumia kwa maslahi mapana ya taifa".

Aliongeza: "Tunawapongeza viongozi wetu wakuu Rais Dk. Samia na Dk. Hussein kwa maono yao na kazi kubwa wanazozifanya kwa maslahi mapana ya wananchi na taifa letu kwa ujumla".

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Juma Makungu Juma, alisema takwimu ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Aliendelea kusema kuwa, ukosefu wa takwimu sahihi ni sawa na kwenda vitani bila silaha lazima utashindwa ndiyo maana viongozi wetu wakuu wanasisitiza matumizi yake.

"Tunapoenda kuelimisha umuhimu wa takwimu itasaidia kutoa elimu kwa wananchi. Na kumekuwa na ushirikiano mzuri kati ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya Tanzania bara (NBS) na Zanzibar kwa maslahi ya taifa," alisema.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema ni maono ya Rais Samia na Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kutoa kipaumbele katika kuendeleza takwimu rasmi nchini.

Alisema: "Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 imeleta heshima kwa sababu ilifanyika kisasa na kwa ufasaha wa hali ya juu kutokana na maono ya viongozi wetu".



Baadhi ya madereva wa bajaji wakiwa kwenye foleni ya kuweka mafuta kwenye kituo cha Puma jijini Dodoma jana, kwa ofa ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (hayupo pichani), ambapo kila Bajaji iliwekewa lita tano ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha Maonesho ya Nanenane Kitaifa yanayotarajiwa kuanzia Agosti 1 hadi 8 mwaka huu, mkoani humo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TFS, TAA kupanda miti milioni moja kila mwaka

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI isiyokuwa ya kiserikali ya TAA kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), zimeanzisha kampeni ya kupanda miti milioni moja kila mwaka mkoani Singida.

Kampeni hiyo inajulikana kama 'Singida Mpya ya Kijani Inawezekana' ambapo lengo lake ni kuunusuru mkoa huo katika hali ya kutokuwa na mvua ya kutosha (ukame).

Mkurugenzi Mtendaji wa TAA, Suphian Juma Nkuwi, alisema hayo juzi wakati wa zoezi la upandaji miti 800 katika Shule ya Msingi Unyianga na Shule ya Sekondari Unyianga katika Manispaa ya Singida.

Nkuwi, alisema kampeni hiyo ambayo imeshaanza kutekelezwa na kufanikisha kupanda miti isiyopungua 5,000 katika Halmashauri ya Wilaya za Ikungi, Mkalama na Itigi ambapo lengo ni kupanda miti milioni moja kwa mwaka.

"Tumeamua kuanzisha kampeni hii ya kupanda miti hii kutokana na Mkoa wa Singida kujulikana duniani kwa miaka mingi kama eneo lenye ukame kutokana na ukataji miti unaosababishwa na shughuli mbalimbali za kibinadamu kwa hiyo tunataka kuondoa dhana hiyo," alisema.

Naye Naibu Meya wa Manispaa ya Singida, Geofrey Mdama, akizungumza wakati wa zoezi hilo aliwataka wananchi hasa wa mkoani humo kumuunga mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika utunzaji wa mazingira na kuhakikisha wanapanda miti kadiri wawezavyo.

"Tumuunge mwanamazingira namba moja Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu anapenda mazingira na anafanya kazi kubwa sana kuleta maendeleo kwenye nchi yetu," alisema.

Kwa upande wake Ofisa Mtendaji Kata ya Unyianga, Hassani Wongoyo, alisema wamejipanga kusimamia sheria zilizopo za usimamizi wa mazingira na kuwahamasisha zaidi wananchi kushiriki kupanda miti ili kuufanya mkoa huo kuwa wa kijani.

Aidha, Mkuu wa Shule ya Sekondari Unyianga, Martin Mwamlima na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Unyianga, Ruth John waliishukuru TAA na TFS kwa kuwezesha zoezi la upandaji miti katika shule zao wakisema ni jambo litakalosaidia shule hizo kuwa na hewa nzuri na mazingira ya kuvutia.

"Tuwape pongezi sana kwa kulifanya hili kwa moyo lakini pia tunawaahidi tutaendelea kuitunza ili ilete faida katika maisha yetu ya kila siku, tunafanya hivyo tukitambua kuwa tunaboresha mazingira yetu ya nchi nzima hasa mkoa wetu wa Singida," alisema Ruth.

Wanafunzi wa Shule ya Msingi Unyianga, Rehema Ezekia na Abdulhalim Mohamed alisema wataitunza miti hiyo.

Alisema: "Miti inazuia mmomonyoko wa udongo, inaleta mvua, tunapata hewa safi lakini pia inatupatia kivuli kizuri cha kupumzikia wakati wa jua, sisi wanafunzi tunashukuru sana kwa kutuletea hii miti tunaahidi tutaitunza kwa umoja na kwa nguvu".





# DCEA: Matumzi dawa za kulevya husababisha machafuko

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

MATUMIZI ya dawa za kulevya yametajwa kuwa miongoni mwa vitu vinavyohatarisha usalama wa taifa, kwamba watumiaji wanakuwa na ujasiri uliopitiliza na kuwa na uwezekano wa kusababisha machafuko.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, aliyasema hayo juzi kwenye kikao kazi cha wadau wa kupambana na dawa za kulevya mkoani Songwe, vikiwamo vyombo vya dola kilichofanyika katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe.

Kamishna Lyimo alisema utafiti unaonyesha kuwa kiwango cha uhalifu kwenye mataifa yaliyoruhusu matumizi ya dawa za kulevya kimeongezeka ikiwamo mauaji, uporaji na maandamano yasiyokuwa na sababu.

Alisema taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa Tanzania ni nchi ambayo kwa sasa inaongoza barani Afrika kwa kupambana na dawa za kulevya na kwamba hata hali ya usalama inachangiwa pia na udhibiti wa dawa hizo.

Aliwataka wadau mbalimbali wa mapambano ya dawa za kulevya kushirikiana hasa katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa mwakani ili kuepusha vurugu.

"Mataifa mengi yaliyoruhusu matumizi ya dawa za kulevya usalama umeshuka kwa kiwango kikubwa sana, lakini sisi tumefanikiwa sana kudhibiti matumizi ya dawa hizi na kumekuwa na msukumo mkubwa sana wa kututaka turuhusu uzalishaji wa baadhi ya dawa ikiwamo bangi kuwa kama zao la biashara," alisema Kamishna Lyimo.

Alisema wamekuwa wakishirikiana na wadau mbalimbali kudhibiti mianya yote ya uingizaji wa dawa za kulevya ikiwamo kuwakamata wasafirishaji na kuwachukulia hatua za kisheria.

Alisema moja kati ya hatua ambazo wahusika wamekuwa wakichukuliwa ni pamoja na kufungwa kifungo cha kati ya miaka 30 na kifungo cha maisha pamoja na kutaifishiwa mali zao.

Alisema hivi karibuni walifanikiwa kukamata zaidi ya kilo milioni 2.5 pamoja na kuwakamata watu mbalimbali wakiwamo mapapa wa dawa za kulevya waliokuwa wameunda mtandao nchi nzima.

Mkurugenzi wa Mradi wa HJFMRI Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Emmanuel Bahemana, alisema mikoa hiyo ni miongoni mwa maeneo ambayo yana idadi kubwa ya waathirika wa dawa za kulevya ambao pia wako katika hatari ya kupata maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Alisema jukumu kubwa la Shirika la HJFMRI ni kupambana na maambukizi ya VVU lakini kutokana na ongezeko la waathirika wa dawa za kulevya lilianza kushirikiana na serikali kukabiliana na janga hilo.

Alisema shirika hilo lilianza mapambano hayo mwaka 2017 ambapo lilishiriki katika kuanzisha kliniki mbili za kuwahudumia waraibu wa dawa za kulevya ambazo moja iko katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe na nyingine iko katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo, aliwataka wadau wote wanaoshiriki kwenye mapambano ya dawa hizo kushirikiana kukabiliana na wimbi la usafirishaji wa dawa hizo.

Alisema wapo baadhi ya wasafirishaji wa dawa hizo kutoka katika mataifa mengine wamekuwa wakitumia hati za kusafiria za Tanzania hali ambayo inalichafua taifa pale wanapokamatwa kwenye mataifa mbalimbali.

Alisema watu hao wanapata hati hizo kwa njia mbalimbali ikiwamo kughushi ama kukaa kwa muda mrefu nchini na hivyo kuanza kuonekana kuwa ni Watanzania.



Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa mamlaka hiyo kwenye kikao cha wadau wa kupambana na dawa za kulevya katika Mkoa wa Songwe juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mamia wamzika mfanyabiashara Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAMIA ya wakazi mkoani Njombe wamejitokeza kwenye mazishi ya mfanyabiashara wa huduma za kifedha, Godfrey Ndambo (45) aliyefariki wakati akipatiwa matibabu Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya.

Mfanyabiashara huyo alifariki dunia baada ya kuvamiwa na majambazi na kupigwa na kitu kizito kichwani akiwa nyumbani na kisha kupora zaidi ya Sh. milioni 47.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ambaye aliwaongoza waombolezaji hao alisema Mkoa wa Njombe umepata simanzi kubwa kwa sababu umepoteza mfanyabiashara mkubwa ambaye alikuwa anafanya vizuri kwenye sekta binafsi.

Alifafanua kuwa matukio ya aina hiyo hayafanywi na watu wa mbali isipokuwa ni watoto, ndugu na marafiki, hivyo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe achukue simu za wanafamilia na watumishi wa marehemu ili kufanyiwa uchunguzi.

Pia alitoa wito kwa wananchi mkoani Njombe kutoa ushirikiano wa taarifa ambazo itasaidia kukamatwa kwa wahusika wa mauaji ya mfanyabiashara huyo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Deo Sanga aliiagiza kamati ya ulinzi na usalama Mkoa wa Njombe kuhakikisha waliohusika na tukio la uvamizi na kusababisha kifo cha Ndambo wanakamatwa ndani ya siku mbili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga alisema katika kipindi cha muda mfupi kuna matukio matano yamejitokeza ya mauaji kwenye maeneo tofauti ya mkoa huo likiwemo la mfanyabiashara huyo.

Alisema katika matukio hayo yote ni tukio mmoja pekee linalomuhusu mfanyabiashara aliyefariki ndiyo watuhumiwa bado hawajapatikana lakini yaliyobaki kuna watuhumiwa wanashikiliwa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Ramandhani, Evaristo Mwimba, alisema wapo vijana ambao wanafanya uhalifu kwenye maeneo ya mtaa huo ambao umri wa ni kati ya miaka 48 na kushuka chini.

Mwakilishi wa familia ya mfanyabiashara huyo, Meshack Ndambo aliwashukuru wananchi mkoani Njombe kwa kuacha shughuli zao na kujitokeza na kushiriki kwenye mazishi ya ndugu yao.

## Viziwi waomba msaada wa alama maalumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wenye ulemavu wa kusikia (viziwi) mkoani Mbeya, wameomba serikali kuwatafutia alama maalumu ya utambulisho wanapokuwa barabarani, ili kuwaepusha na ajali zinazoweza kugharimu maisha yao ama kuwasababishia ulemavu mwingine wa viungo.

Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Mkoa wa Mbeya, Tusajigwe Mwalweja, alitoa ombi hilo juzi kwenye mkutano ulioandaliwa na Chama cha Watu wenye Ulemavu mkoa wa Mbeya (SHIVYAWATA) uliofanyika katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Alisema serikali imefanya maboresho mbalimbali ya huduma kwa watu wenye ulemavu ikiwamo kuajiri wakalimani wa lugha ya alama na fimbo nyeupe kwa watu wasioona.

Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona mkoa wa Mbeya na Songwe, Yohana Mwonga, aliomba walemavu kushirikishwa kwenye mikutano inayofanyika katika maeneo yao kwa maelezo kuwa wana haki ya kutoa maoni na kufahamu yanayoendelea katika jamii zao.

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk.Godlove Mbwanji, alisema serikali inaendelea kufanya uboreshaji wa miundombinu rafiki kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya kwa makundi maalumu.



# Waziri Othman ataja siri kulifufua zao la mwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Shaban Ali Othman, amesema kuwapo kwa sera nzuri ya zao la mwani ndiyo chanzo cha kuliongezea thamani zao hilo.

Akizungumza jana katika kilele cha siku ya mwani visiwani hapa, waziri huyo alisema licha ya kuwapo kwa sera ya uchumi wa bluu na uvuvi, lakini sera hiyo imeonekana kulibagua zao la mwani.

Alisema kuwa wakulima wa zao hilo wamekuwa wakithamini juhudi zinazofanywa na serikali za kuongeza bei na thamani ya zao ili wakulima kupata tija kupitia zao hilo.

Alisema katika kuhakikisha kuwa zao hilo linakuwa mhimili mkubwa kwa wakulima Serikali ya Zanzibar tayari imeshaanzisha kampuni ya mwani pamoja na kujenga kiwanda cha kusarifu zao hilo.

Waziri Shabani alisema kuwa katika kuhakikisha mnyororo wa thamani unaongezeka kwa wakulima wa mwani tayari serikali imeshafungua njia kwa kujenga kiwanda cha kusarifu mwani eneo la Chamanangwe Pemba, ambacho kitaanza kazi hivi karibuni.

Alisema kuwa wakati umefika kwa wadau wa sekta ya mwani kuelekeza jitihada za kuzalisha kwa ngazi ya viwanda ikiwamo chakula cha mifugo na mbolea.

Alisema hatua hiyo itanufaisha mazingira ya baharini kwa kusaidia kuondoa virutubisho, kutoa makazi na chakula cha samaki, kusaidia kupunguza hewa ukaa.

Aidha, alisema kuwa mbegu za zao la mwani zimeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi, hivyo wanaendelea na utafiti ili kupata vitalu vya mbegu zinazohimili changamoto hiyo.

Alisema kuwa zao la mwani linakabiliwa na changamoto ya athari ya mabadiliko ya tabianchi katika ukuaji wake, hivyo ni wajibu wa kila mtu kuilinda bahari na kutunza mazingira.

Alisema kuwa wadau wa sekta ya mwani wanapaswa kuendelea kuwahamasisha vijana wa kiume kujiajiri katika sekta hiyo, ili kupunguza tatizo la ajira kwasababu asilimia kubwa ya waliomo kwenye sekta hiyo bado ni wanawake watu wazima.

Mwenyekiti na mwezeshaji wa kongamano la mwani Zanzibar, Dk. Flower Msuya, alisema hivi sasa wanawake wengi wanamwamko wa kulima kilimo hicho kwa vile wamejengewa uwezo na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya Zanzibar.

Ofisa miradi wa Taasisi ya Milele Foundation, Khadija Shariff, alisema wataendelea kutoa elimu kwa wakulima wa zao hilo hasa kwa vijana ili kuongeza ushiriki wao katika kilimo hicho badala ya kuwaachia wanawake pekee.



Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa (katikati waliosimama), akikagua zoezi la usajili katika mfumo wa kielektroniki wa kadi za uanachama wa CCM katika Tawi la CCM Muembeshauri Unguja juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Serikali yawatangazia kiama mawakala makanjanja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein amesema serikali itawachukulia hatua za kisheria mawakala walioshindwa kujisajili, vyuo vyao kushindwa kutambulika.

Aliyasema hayo juzi wakati akifunga maonesho ya tano ya wiki ya elimu ya juu, yaliyofanyika viwanja vya Maisara Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema hivi sasa kumeibuka vijana wengi kukusanya wanafunzi na kuwasafirisha kwenye vyuo ambavyo havina sifa na vyeti vyao havitambuliki nchini, jambo ambalo ni kinyume na taratibu za nchi.

Aidha, aliwataka wazazi, walezi na wanafunzi wanaotafuta fursa za masomo kutumia mawakala wanaotambulika na serikali sambamba na kuwafichua mawakala wababaishaji.

"Nasema wazi jambo hilo halikubaliki na sisi kama serikali tunalifuatilia kwa karibu kuwakamata watu hao, ni vyema wazazi na walezi kufuatilia kwa karibu mawakala kabla ya kulipia fedha nyingi bila ya kujua kuwa wapo kisheria," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau kutumia fursa zinazopatikana nchini kwa lengo la kuboresha sekta ya elimu ikiwamo kuongeza fedha katika mfuko wa elimu ya juu.

Kadhalika, alisema wizara itaongeza maboresho kwa maonesho yanayokuja katika eneo la huduma, kupunguza bei ya mabanda na kutoa matangazo zaidi kwa vyombo vya habari ili wananchi wengi wapate uelewa.

Alisema kuwa serikali imejipanga kufanyia kazi changamoto zote zilizojitokeza katika maonesho hayo, ili yanayokuja kuwa na mafanikio zaidi na kuleta manufaa makubwa.

Mkuu wa Kitengo cha Uratibu Elimu ya Juu Zanzibar, Aida Maulid, alisema miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika maonesho hayo ni kuongeza idadi ya washiriki kutoka 54 ya mwaka jana hadi 77 mwaka huu.

# Rais mstaafu Karume asisitiza uwekezaji katika vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume, amesema ili kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani kunahitajika uwekezaji utakaowawezesha vijana kuwa na ujuzi.

Dk. Karume alisema hayo katika hafla ya utiaji saini hati za makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya sayansi na teknolojia kati ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST) na Chuo Kikuu cha Teknolojia IIT Madras cha India, Kampas ya Zanzibar.

Dk. Karume ambaye ni Mkuu wa MUST, alisema hatua hiyo itasaidia vyuo hivyo kuwa na ushirikiano katika masuala ya utoaji wa taaluma ya teknolojia ili kwenda sambamba na dunia.

Alisema ulimwengu sasa unatawaliwa na sayansi na teknolojia, hivyo kuunganishwa kwa vyuo hivyo katika masuala ya taaluma itasaidia vijana kuwa na uelewa mpana katika masuala ya teknolojia na kufanya mageuzi makubwa ya kiuchumi nchini.

Aidha, alitumia fursa hiyo kuvitaka vyuo hivyo kufundisha vijana kuwa wavumbuzi na kujitegemea wenyewe badala ya kuwa mzigo kwa taifa na familia zao pindi wanapohitimu masomo yao.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa, alisema ushirikiano wa vyuo hivyo utasogeza karibu fursa za kupata wataalamu ambao watatumika katika viwanda ubunifu na miundombinu ndani ya nchi na Afrika.

Alisema Chuo cha IIT ni wabobezi katika fani ya teknolojia na uvumbuzi hivyo hatua hiyo itasaidia kuzaa matunda chanya ndani na nje ya Tanzania ambapo miongoni mwa malengo na mikakati ya serikali ni kufanya Zanzibar kuwa kituo cha vyuo vikuu vya kitaifa na kimataifa.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Prof. Aloys Mvuma, alisema ushirikiano huo unaenda sambamba na makubaliano na mahitaji ya nchi kwa kuwa itasaidia kuimarisha huduma za teknolojia katika utoaji wa elimu nchini.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuboresha mifumo ya kufundishia katika masuala ya teknolojia na utafiti ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ASMAA KHAMSWAN KIMARO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASSPORT NO, **TAE 279223** ILIYOTOLEWA NA OFISI YA UHAMIAJI 13 JAN 2020 DAR ES SALAAM. YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA: **PHQ/ KIL/MOS/16539/2024**

## KUPOTEA NYARAKA UMILIKI VIWANJA

**MUSA JIHANGO TUNGU**

anatangaza kupotelewa na nyaraka za umiliki wa viwanja namba 82 na 84 Kitalu "NN" vilivyopo Ndala Manispaa ya Shinyanga

kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu

TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/SHI/SHI/5946/2024**

---

JAMUHURI YA MUUNGANO TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA

Simu ya upepo "MKUU PO/MJINI
Simu: 2230771 / 2 Ext.9
Dir, 2231368
Fax 02242237666
Email polisimjinimagharibi@gmail.com

Ofisi ya Mkuu wa Kituo
kituo cha Polisi Madema
Sanduku la Posta 237,
Zanzibar

## WITO WA POLISI

**NDUGU SALIM SHAIR AHMADA**
**WA KIJICHI**
**22/07/2024**



Husika na mada tajwa hapo juu,
Unatakiwa kufika kituo cha polisi Madema siku Alhamis ya tarehe 25/7/2024 majira ya saa 8:00 wakati wa ASUBUHI na ukifika kituoni hapo unatakiwa kuonana na OCD wa MADEMA polisi Madema. Kufika kwako ni muhimu kwasababu kuna jambo muhimu linalohusika na MAD/RB/110/2024 ambalo linakuhusu.
Ni wajibu wako kutii sharia ya shurti.

MKUU WA KITUO CHA POLISI
MADEMA
Mkuu wa kituo
Kituo cha Polisi Madema

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA 13 LA MWAKA2023**

**(Asilia kutoka Baraza la Ardhi,Nyumba na Maendeleo LA Wilaya ya Mbeya,Maombi Nambari 198 ya mwaka2019)**

**GODWIN MASAGA...............................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**BAHATI MWATEGA............................MRUFANIWA WA 1**
**HOMANGE CASTORY (msimamizi wa Mirathi ya CHARLES NGAO).........................MRUFANIWA WA 2**

**KWA: BAHATI MWATENGA**

**POPOTE MLIPO**
**KUITWA SHAURINI**

Unaarifiwa na Mahakama hii,kuhudhuria hapa Mahakamani binafsi au Wakili wako tarehe 22/08/2024 siku ya Alhamisi saa3:00 kamili asubuhi,ambapo shauri limepangwa kusikilizwa. **ELEWA KWAMBA,** ukikosa kufika siku hiyo,shauri litapangwa kusikilizwa bila wewe kuwepo.
Hati imetolewa kwa Mkono wangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 17/ 07/2024.

17/07/20..
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**

**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......42/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: IDD KASSIM Wa K/NDEGE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA: HANIFA AZIZI**

### TANGAZO

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 05 Mwezi 09 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehem anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 07 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NAMBA 81 YA 2024**

**ABDALLAH JUMA MIKONZI (Msimamizi wa mirathi ya Juma Abdalla Mikonzi).......................................................MLETA MAOMBI**

### WITO/KUITWA SHAURINI KWA

1. **NEMESI VICTORY MKUDE**
2. **SARA MTAMBUKA**
3. **PASKARI BLASI KENGE**
4. **ASMA MKEYE**
5. **CENTER FOR COMMUNITY INITIATIVE**
6. **TANZANIA FEDERATION FOR URBAN POOR**
7. **IMANI DAUDI**
8. **NEEMA SALUM**
9. **MAMELTA JOHN.......................................MJIBU MAOMBI**

Popote mlipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 07/08/2024 mbele ya Mwenyekiti M.KHASIM nyie wenyewe au mtume muwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 23 mwezi July, 2024.

M. KHASIM
MWENYEKITI.
MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA ... WILAYA YA MOROGORO TANZANIA

---

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA.**

**LILILOPO MASWA.**

**MAOMBI MADOGO NA. 37 YA MWAKA 2024**
**{Arising from DLHT at Maswa Appl no 44/2023}**

**KATI YA THE BOARD OF TRUSTEES OF ISLAM BAKWATA..............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**SULEIMAN LUGWISHA......MJIBU MAOMBI**

**WITO/TAARIFA**
**Kwa: SULEIMAN LUGWISHA POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yako katika Baraza hili la wilaya ya Maswa,maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi kabla ya tarehe 16.08.2024.
Pia unajulishwa kuwa shauri hili limepangwa kutajwa siku ya tarehe 26.08.2024 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Maswa.
Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakadi wito huu na kushindwa kuleta utetezi wako wa maandishi kwa muda uliopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza shauri hili upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 16.07.2024

J.T.KAARE
MWENYEKITIBARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MASWA
MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA TANZANIA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 17105 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE SAMWEL MDOE MAGEMBE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY VALENTINO SAMWEL MAGEMBE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 22th day of August, 2024.
Dated at Korogwe this 22th day of July, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kamala Harris afufua matumaini ya Democrat

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, amefufua matumaini ya Chama cha Democrat, baada ya kufanya kampeni yake ya kwanza iliyowasisimua wapigakura wengi.

Harris alimrushia maneno mgombea wa Republican, Donald Trump, akimuita mnyanyasaji wa kijinsia na kueleza uchaguzi mkuu utakaofanyika Novemba mwaka huu watu watachagua kati ya mwendesha mashtaka wa zamani na mhalifu aliyepatikana na hatia.

Akizungumza na umati wa watu wapatao 3,000 katika eneo la jimbo lenye ushindani la Wisconsin, Harris alimfananisha mpinzani wake huyo ambaye alikuwa rais wa taifa hilo, kuwa ni mlaghai aliyowahi kumfungulia mashtaka.

Hata hivyo, Trump, alijibu mapigo kwa kumshambulia Harris kwa rekodi yake ya utendaji kwenye mpaka.

Trump alichapisha kwenye mtandao wa kijamii wa X kuwa Kamala Harris anaharibu kila kitu anachogusa!

Kampeni ya Harris ilianza baada ya kupata uungwaji mkono wa wajumbe wengi wa chama chake cha Democrat, na kumtengenezea njia ya kuwa mgombea mteule wa chama hicho.

Kampeni ya Harris ilichangisha kiasi cha dola milioni 100 katika muda wa saa 36 baada ya Rais Joe Biden kutangaza kujiuzulu.

Katika matokeo ya kura za maoni kuhusu uchaguzi uliofanywa na mashirika ya habari la Reuters na Ipsos zinamwonyesha Harris akiwa mbele kwa asilimia 44 dhidi ya Trump, aliyepata 42.

Utafiti huo ni wa kwanza kufanywa tangu Rais Joe Biden alipojiondoa katika kampeni ya kugombea muhula wa pili. Kura hiyo ya maoni ilifanyika kwa siku mbili baada ya Biden kutangaza kujiondoa kwenye kinyang'anyiro na kumpendekeza makamu wake wa rais.

Katika uchunguzi wa maoni wa wiki iliyopita, Harris mwenye umri wa miaka 59, na Trump (78), walikuwa wote na asilimia 44.

Makamu huyo wa rais anayepigiwa upatu na Wanademocrat wengi anaendelea kuungwa mkono na vigogo na kupata michango mingi.

***BBC***



Raia wa Nepal wakiangalia mabaki ya ndege iliyoanguka na kuua watu 18 jana. **PICHA: REUTERS**

# Wanahabari waandamana Kenya

**NAIROBI,** KENYA

WAANDISHI wa habari nchini Kenya, wamefanya maandamano kupinga vitendo vya ukatili, vitisho vinavyofanywa na polisi na kusababisha maisha yao kuwa shakani.

Maandamano hayo yamefanyika katika Jiji la Nairobi na yameandaliwa chini ya mwamvuli wa Chama cha Wahariri wa Kenya (KEG), pamoja na Muungano wa Wanahabari wa Kenya (KUJ) na wadau wengine 20 wa sekta ya habari.

"Wanahabari wote na watetezi wa haki za binadamu wanalaani mashambulizi na unyanyasaji unaowalenga wanahabari na vitisho vyote kwa uhuru wa vyombo vya habari kama inavyothibitishwa na Katiba yetu," ilisema taarifa ya wahariri hao.

Walieleza kukamatwa kwa mwanahabari mkongwe Macharia Gaitho, Julai 17, mwaka huu na baadaye polisi ilikiri kumshikilia ni jambo lisilo sahihi.

Pia waandishi hao walipinga kitendo cha kupigwa risasi kwa Catherine Wanjeri Kariuki, ambaye ni mtangazaji wa televisheni na redio mjini Nakuru.

"Leo, wafanyakazi wa vyombo vya habari wanatumia haki zao kama raia na wanataaluma kujumuika pamoja na kuonyesha hasira zetu kuhusu unyanyasaji wa polisi dhidi ya waandishi wa habari, "Alisema Ruth Nesoba ambaye ni naibu rais wa chama cha wahariri nchini humo (KEG).

Aliongeza "Vitisho vya kufunga makampuni ya vyombo vya habari, na mbinu nyingine za kizamani zinazotumiwa na mashirika ya serikali na wanasiasa wanaotaka kuzuia uhuru wetu tulioupata kwa bidii ni jambo lisilokubalika," Maandamano hayo yaliishia katika jengo la Jogoo House na kuwasilisha malalamiko yao kwa Kaimu Inspekta Jenerali Douglas Kanja na kisha kuelekea Teleposta Towers kuwasilisha ombi kama hilo kwa Wizara ya Habari na Mawasiliano.

Wakati huo huo, Rais William Ruto aliwatangaza mawaziri wengine 10 wakiwamo viongozi wa kambi ya upinzani kuunda serikali mpya.

Rais Ruto aliwarejesha mawaziri wa zamani wanne ambao waliokuwa katika baraza lake la hapo awali ambalo lilivunja.

Walioteuliwa kushika nafasi hizo ni John Mbadi (Wizara ya Fedha), Salim Mvurya (Uwekezaji), Rebecca Miano (Utalii), Opiyo Wandayi (Nishati), Kipchumba Murkomen (Vijana na Michezo), Hassan Joho (Madini) na Alfred Mutua (kazi).

Wengine ni Wycliffe Oparanya (Vyama vya Ushirika),Justin Muturi (Utumishi wa Umma) na Stella Langat (Jinsia).

***TRT.***

## Kiongozi DRC atenguliwa baada kukutana na M23

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, ametengua nafasi ya Jean-Bosco Bahala, kuwa mratibu wa Mpango wa Kupokonya Silaha na kuwarejesha wapiganaji katika maisha ya kiraia (PDDRC-S).

Hatua hiyo ilichukuliwa juzi baada ya kiongozi huyo kushiriki katika mkutano wenye utata wa kutafuta amani nchini Uganda.

Mkutano huo ambao ulifanyika siku moja kabla, uliwahusisha wajumbe kutoka jukwaa la Alliance Fleuve Congo (AFC) na waasi wa M23.

Ingawa Jean-Bosco Bahala alikanusha kushiriki mkutano wowote na wajumbe wa jukwaa la Alliance Fleuve Congo, AFC, akidai kwamba alikuwa Uganda kwa ajili ya kuwarejesha makwao watoto wa DRC walioachiliwa na waasi wa LRA Serikali ya DRC ilisema haijaagiza mtu yeyote kwenda Entebbe kujadiliana na AFC.

Kulingana na taarifa kutoka RFI, Jean-Bosco Bahala alishiriki katika mkutano huo chini ya uwezeshaji wa serikali ya Uganda.

Mkutano uliisha bila kupata muafaka, na Bahala aliondoka katikati ya majadiliano.

Hata hivyo, kesi dhidi ya kiongozi wa AFC, Corneille Nangaa, na washirika wengine wa mwenyekiti wa zamani wa Tume ya Uchaguzi (CENI), ilifunguliwa jana katika Mahakama ya Kijeshi ya Gombe.

Kulingana na Wizara ya Sheria, kesi hiyo ambayo watuhumiwa hawakuwapo mahakamani wanakabiliwa na mashtaka ya kufadhili ugaidi, uhalifu wa kivita na uhaini dhidi ya serikali.

***RFI***

**Mkutano huo ambao ulifanyika siku moja kabla, uliwahusisha wajumbe kutoka jukwaa la Alliance Fleuve Congo (AFC) na waasi wa M23.**

# DODOMA JIJI FC YATAKA MECHI TANO ZA KIRAFIKI

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa klabu ya Dodoma Jiji FC, umesema kuwa unatarajia kucheza michezo mitano ya kirafiki katika maandalizi yao ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Klabu hiyo, Johnson Fourtnatus amesema michezo hiyo itawasaidia kukiimarisha kikosi chao pamoja na kutoa fursa kwa benchi la ufundi kuona mapungufu na kuyafanyia kazi.

„Timu yetu kwa sasa ipo mkoani Arusha kwa ajili ya kambi, malengo yetu tunataka kabla msimu haujaanza tucheze michezo hiyo kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa wachezaji wetu,“ alisema Fourtnatus.

Aidha, alisema wamejiwekea malengo ya kumaliza katika nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu na kuomba mashabiki wao waendelee kuiunga mkono timu yao.

Katibu huyo alisema wiki ijayo watatangaza wachezaji ambao wamewasajili pamoja na wale watakaowaacha kwa ajili ya kuboresha kikosi chao kuelekea msimu ujao.

Kwa upande wake Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mecky Maxime, alisema timu yake inaendelea vizuri na mazoezi kuhakikisha msimu ujao wanatimiza malengo waliyojiwekea.

Aliongeza kwa kusema kuwa, kila mchezaji ana morali ya juu na anachokifanya kwa sasa ni kuwapa mbinu ambazo zitawasaidia kupambana na wapinzani ndani ya uwanja.



Kocha wa mpira wa kikapu, Hadija Karambo (kulia), akimwonesha mfano wa kurusha mpira kwa mkono mmoja mchezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya Vijana, Gradnes Komba, wakati wa mazoezi yaliofanyika kwenye Uwanja wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Tuzo wachezaji bora Ligi Kuu Agosti Mosi

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi wanatarajia kutoa tuzo za wachezaji bora kwa timu zilizofanya vizuri msimu uliopita, zitakazofanyikia jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa jana na TFF, inaeleza kuwa tuzo hizo zitatolewa kwa mujibu wa uteuzi wa Kamati ya Tuzo ambayo imeshafanya kazi hiyo kwa kuchagua wachezaji na timu zinazostahili kupata tuzo hizo.

Taarifa imesema kwa mara ya kwanza, kamati hiyo imeongeza tuzo tatu ambazo hazikuwapo kabla ambazo ni tuzo ya mchezaji bora wa Kitanzania anayecheza nje ya nchi kwa upande wa wanaume, mchezaji bora wa kike anayecheza soka la kulipwa nje ya nchi, pamoja na mchezaji bora wa soka la ufukweni.

Baadhi ya walioteuliwa kuwania tuzo hizo kwa mujibu wa Kamati ya Tuzo ni tuzo ya golikipa bora ambayo itawaniwa na Ayoub Lakred kutoka Simba, Djigui Diarra wa Yanga na Ley Matampi wa Coastal Union. Tuzo nyingine ni beki bora ambayo itawaniwa na Kouassi Yao na Ibrahim Hamad ‚Bacca' kutoka Yanga na Mohamed Hussein ‚Tshabalala' kutoka Simba.

Upande wa kiungo bora walioteuliwa ni Stephane Aziz Ki wa Yanga, Feisal Salum na Kipre Junior wote kutoka Azam FC.

Nafasi ya mchezaji bora wa mwaka wapo, Aziz Ki, Diarra na Bacca wote wa Yanga, Tshabalala wa Simba, Fei Toto na Kipre (Azam), Matampi wa Coastal, huku tuzo ya Kocha Bora ikiwaniwa na David Ouma wa Coastal Union, Bruno Ferry wa Azam FC na Miguel Gamondi wa Yanga.

Aidha, kwenye soka la wanawake nafasi ya mchezaji bora inawaniwa na Ausha Mnunka, Vivian Corazone na Vaileth Nicholaus (Simba Queens), Stumai Abdallah kutoka JKT Queens, na Kaeda Willson wa Yanga.

Kipa bora wa wanawake inagombaniwa na Najath Abbas wa JKT Queens, Caroline Rufa wa Simba Queens na Mariam Shaaban wa Bunda Queens, huku Juma Mgunda wa Simba Queens, Ester Chabruma wa JKT Queens na Burito Mgosi wa Bunda Queens wakiwania tuzo ya ukocha bora wa mwaka.

# SHIME ATANGAZA KIKOSI CHA WACHEZAJI 30

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wasichana wenye umri chini ya miaka 17, Bakari Shime, ametangaza kikosi cha wachezaji 30 kitakachoingia kambini Julai 29 kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya UNAF yatakayofanyika nchini Tunisia.

Shime, aliwataja wachezaji hao kuwa ni Mariam Shabani, Melkia William, Kurwa Rocket, Semeni Juma, Ester Maseke na Jamila Selestine wote kutoka klabu ya Bunda Queens.

Wengine ni Jamila Rajab, Winfrida Gerald, Mwatima Mwarabu, Yasinta Mitoge na Lydia Maximillian kutoka klabu ya JKT Queens.

Wachezaji wengine ni Sarah Joel, Manka Richard na Merry Siami kutoka Fountain Gate.

„Wachezaji wengine ambao nimewajumuisha kwenye kikosi ni Masika Mwakisua, Winfrida John kutoka Yanga Princess na Odiliya Bakajibana na Sundi Ramadhani kutoka The Tiger Queens", alisema Shime.

Aliwataja wachezaji wengine kuwa ni Mtundagi, Jesca Jeremia, Furaha Kifaru (Bilo Queens), Naomi Charles, Sabina Alex, (Geita Queens).

Bahati Hamis (Umiseta Mara), Neema Thomas (Singida), Nusra Hamis (Alliance Girls), Agatha Lupembe (Mlandizi Queens), Nora Mushi (Oysterbay) na Devotha Julius (Umiseta Tabora).

## ZISIKUPITE

### MOUNT KUPIGWA BEI
KLABU ya Manchester United ipo tayari kumuuza kiungo wa kati wa England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 25, msimu huu wa majira ya joto. ***(HITC)***

### RABIOT KUTUA MAN U
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, anakaribia kusaini Manchester United baada ya kuondoka Juventus mwishoni mwa mkataba wake. ***(Mail)***

### SETFORD AWANIWA ARSENAL
ARSENAL inajiandaa kumsajili mlinda mlango wa Uingereza, Tommy Setford mwenye umri wa miaka 18 kutoka Ajax kabla ya ziara yao ya kwenda Marekani. ***(Evening Standard)***

### LINDSTROM KWA MKOPO
KIUNGO wa kati wa Denmark, Jesper Lindstrom mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kucheza kwa mkopo wa msimu mzima pale Everton kutoka Napoli. ***(CalcioMercato)***

### DIEGO GOMEZ AWINDWA
KLABU ya Brighton imefanya mazungumzo na Inter Miami kuhusu mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Paraguay, Diego Gomez mwenye umri wa miaka 21.***(Sky Sports)***

### HARRIS AWANIWA BIRMINGHAM
KLABU ya Birmingham City imeelekeza macho yao kwa kiungo wa Fulham na Wales, Luke Harris mwenye umri wa miaka 19. ***(Football Insider)***

### ARSENAL YAKOMAA NA CALAFIORI
ARSENAL imeongeza juhudi zao za kumsajili beki wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22, kutoka Bologna. ***(The Athletic)***

### KANTE KUTUA WEST HAM
KLABU ya West Ham imefikia makubaliano ya mdomo ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 33 kutoka Al Ittihad. ***(The Athletic)***

### LUCAS DIGNE KUUZWA
ASTON Villa inajiandaa kumuuza mlinzi wa Ufaransa, Lucas Digne mwenye umri wa miaka 31. ***(Football Insider)***

### UGARTE SAFI NA MAN
KIUNGO wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte mwenye umri wa miaka 23, amekubaliana maslahi binafsi na Manchester United, ambao wanaendelea kufanya mazungumzo na PSG. ***(Fabrizio Romano)***

### MCTOMINAY AWEKEWA BEI
MANCHESTER United imeweka bei ya pauni milioni 30 kwa kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL KUMBAKIZA SMITH ROWE EMIRATES

Washikabunduki hao wamekataa ofa ya Fulham ya kutaka kumnunua mchezaji huyo lakini...

**LONDON, England**

ARSENAL inajiandaa kumbakisha nyota wake, Emile Smith Rowe msimu huu wa majira ya joto baada ya kukataa ofa kutoka kwa Fulham, lakini inasemekana hawatamzuia mchezaji huyo ikiwa ataonesha nia ya kuondoka kama itapata ofa inayofaa.

David Ornstein aliripoti kuwa klabu hiyo ya Kaskazini mwa London ina wachezaji ambao wangependelea kuwauza mbele ya kiungo huyo, ingawa hakuweza kumtaja mtu yeyote.

Kulingana na Ornstein, „Arteta anasalia kuwa shabiki mkubwa wa mchezaji huyo, na klabu haijavutiwa sana na viungo wanaopatikana sokoni msimu huu wa majira ya joto."

„Matakwa ya mchezaji yanaweza kuwa sababu ya kuamua. Ikiwa Smith Rowe ataonesha nia thabiti ya kuondoka na Arsenal ikapokea ofa inayofaa, klabu haitaweza kumzuia."

Arsenal ilikataa ombi la Fulham kwa Smith Rowe wiki hii huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 akiripotiwa kufikiria mustakabali wake.

Matatizo ya jeraha la kiungo huyo yamemfanya ashindwe kupata dakika za kutosha, gazeti la The Athletic liliripoti kwamba uhamisho ungetokana na nia ya mchezaji huyo kutaka kucheza kikosi cha kwanza.

Mashabiki wanampenda Smith Rowe sio tu kama bidhaa ya Hale End Academy, lakini pia kwa uchezaji wake katika msimu wa Ligi Kuu wa 2020/21.

Arteta alimleta mchezaji huyo kwenye kikosi chake dhidi ya Chelsea wakati timu ilipopitia kipindi kibaya cha Krismasi.

Smith Rowe alikuwa sehemu muhimu ya timu hiyo ya Arsenal msimu uliofuata kabla ya majeraha na usajili wa wachezaji wapya waliosajiliwa vimechangia kwa kiasi kikubwa kuporomoka kwa mchezaji huyo katika ubora wake.

Smith Rowe amecheza mechi 25 pekee katika misimu miwili iliyopita.

Smith Rowe alitajwa kwenye kikosi cha wachezaji 26 cha Arsenal kwa ajili ya ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya Marekani pamoja na Reiss Nelson na Eddie Nketiah ambao pia wamehusishwa kuondoka Arsenal.

# BENZEMA AMPA VINICIUS BALLON D'OR 2024




**PARIS,** UFARANSA

MCHEZAJI wa zamani wa Real Madrid, Karim Benzema, amesema nyota wa timu ya taifa ya Brazil na Real Madrid, Vinicius Junior 'Vini Jr' anastahili kushinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka 2024 'Ballon d'or' inayotolewa na gazeti la Ufaransa.

Kupitia Marca, Benzema alisema Vini Jr alikuwa na msimu mzuri na mabingwa hao wa Ulaya na Hispania.

"Ninaweza kusema Vini Jr anastahili kubeba tuzo ya Ballon d'or kwa mwaka huu, kwa sababu amekuwa na mchango mkubwa katika timu yake," amesema Benzema.

Msimu wa 2023/24 katika Ligi Kuu ya Hispania Vini Jr alifunga mabao 15 katika mechi 26 na akiwa amefunga mabao sita na kupiga pasi nne za mabao katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Benzema ambaye anacheza katika timu ya Al Ittihad ya Saudia Arabia aliwahi kushinda tuzo ya Ballon d'or mwaka 2022 baada ya kuisaidia Real Madrid kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu nchini Hispania.

# Man City yaanza ziara na kichapo



**NORTH CAROLINA,** MAREKANI

KLABU ya Manchester City ilipoteza kwa mabao 4-3 kutoka kwa Celtic katika mchezo wa kwanza wa ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani Jumanne usiku.

Kocha Pep Guardiola aliwachagua Erling Haaland na Jack Grealish katika timu yake, lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu England walifungwa na mabingwa wa Scotland huko North Carolina.

Celtic, ambao walimchezesha kwa mara ya kwanza mlinda mlango Kasper Schmeichel, walitumia fursa ya kuwa mbele zaidi katika maandalizi ya msimu mpya kwa kuongoza kwa bao lililowekwa kimiani na Nicolas-Gerrit Kuhn.

Oscar Bobb aliisawazishia City kabla ya Celtic kufunga mabao mawili kuelekea mwisho wa kipindi cha kwanza yakifungwa na Kuhn na Kyogo Furuhashi.

Muajentina Máximo Perrone akitokea benchi kwa City wakati wa mapumziko na alifunga bao kwa timu ya Guardiola sekunde chache tu baada ya kipindi cha pili.

Bobb alitoa asisti nyingine alipopiga krosi kwa Haaland, ambaye alianza usiku kama nahodha na kufunga bao la tatu la City kabla ya Luis Palma aliyetokea benchi kufunga bao la nne na kuwafanya Celtic kuwa mbele.

City wana mechi zaidi Marekani dhidi ya AC Milan na Barcelona huku Celtic wakianza kampeni yao ya Ligi Kuu ya Uskoti kwa mchezo wa nyumbani dhidi ya Kilmarnock Agosti 4.

## Williams aonywa usajili kwenda Barca

**BARCELONA,** HISPANIA

MCHEZAJI anayesakwa zaidi na Barcelona, Nico Williams ameonywa dhidi ya uhamisho wa hadhi ya juu kwenda Camp Nou na mchezaji mwenzake wa Athletic Club, Oscar de Marcos, akisisitiza kwamba anahitaji kufanya uamuzi wake mwenyewe na sio kuongozwa na shinikizo au matarajio.

Williams amekuwa mchezaji wa kikosi cha kwanza huko Bilbao kwa miaka mitatu, lakini maisha yake ya soka yalizidisha kasi katika michuano ya hivi majuzi ya Ulaya akiwa na Hispania.

Arsenal na Chelsea zimehusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ambaye upatikanaji wake unawezekana kwa dau la euro milioni 58, lakini ni Barcelona ambao ndio wenye nafasi kubwa.

Rais wa Barca, Joan Laporta tayari amekejeli kwa kuwaambia mashabiki "tutajaribu" alipoulizwa kama klabu hiyo itamsajili Williams.

"Inaonekana kama kuna wimbi kwamba wakati Barca inakuhitaji, lazima uende, vinginevyo unafanya makosa, lakini mara nyingi unapaswa kukumbuka kuwa sio kila kitu kinachong'aa ni dhahabu," alisema De Marcos kupitia Mundo Deportivo.

"Lazima ujitathimini ulipo, kwa Nico ni hali tete, kuna kelele nyingi, inaonekana shinikizo hili linaweza kukupata, lakini kila mmoja anatakiwa kufanya maamuzi kivyake, ni mchezaji wa Athletic, atakuwa na neno la mwisho, tunaamini kwamba atakaa pamoja nasi."

De Marcos aliendelea, "Lazima ufanye maamuzi mwenyewe. Sijui anachofikiria. Lazima atakuwa anapitia mambo kichwani mara elfu. Maoni yangu ni kwamba jambo bora kwake ni kuendelea.

"Ana umri wa miaka 22, yuko mahali sahihi kuendeleza maendeleo bora kwa mwanasoka. Kila mwaka anazidi kuwa bora, yuko na kocha ambaye amepata mengi zaidi kutoka kwake na ambaye ataendelea kwa mwingine.

"Amekwenda timu ya taifa, amekuwa mmoja wa wachezaji bora katika michuano ya Ulaya, yuko mahali pazuri, kwenye chumba cha kubadilishia nguo cha ajabu, kaka yake Inaki yupo pamoja naye.

"Ni mahali pazuri pa kuendelea kukomaa na ana hisia za kuwa wa Athletic. Natumaini ataweka kila kitu kwenye mizani, lakini kitu pekee tunachotaka ni bora kwake. Kinachonitia wasiwasi zaidi ni kwamba anafanya uamuzi mgumu, mwenyewe nina mapenzi mengi kwake, nataka afanye uamuzi kwa uhuru na kwa njia hiyo atafanya sahihi.

# WAZIRI MKUU MAJALIWA AITA WAFANYABIASHARA AFCON

**Na Faustine Feliciane**

KUFUATIA Tanzania kuwa mwenyeji mwenza wa fainali za Mataifa ya Afrika AFCON mwaka 2027, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wafanyabiashara kuchangamkia fursa ya kuwapo kwa fainali hizo hapa nchini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Majaliwa alisema kuwapo kwa fainali hizo ni fursa kibiashara na kuwataka wafanya biashara wa sekta binafsi kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali ili kuzishawishi nchi nyingi kuja kukaa Tanzania kwa ajili ya fainali hizo.


"Fainali hizo pamoja na mambo mengine lakini hii ni fursa ya kibiashara, wenzetu nao tunaoandaa nao pamoja wanafanya mipango ya kuvutia nchi nyingi kwenda kwao, nitoe wito kwa wafanyabiashara wetu kuchangamkia fursa hii," alisema Majaliwa.

Aidha, alisema serikali inajithaidi kuboresha miundombinu ya uwanja ili kuweza kushawishi timu kuja kufanya mazoezi hapa nchini wakati wakijiandaa na fainali hizo.

"Tutaboresha uwanja wa CCM Kirumba, Uwanja wa Majimaji Songea, Uwanja wa Uhuru na Fumba Zanzibar, lengo ni tuvutie mechi nyingi zichezwe Tanzania," alisema.

Alishauri wafanyabiashara kuwekeza kwenye sekta ya hoteli, chakula na usafirishaji kwa kuwa fainali hizo ni fursa kubwa ya kibiashara.

Tanzania itashirikiana kwa pamoja na nchi za Kenya na Uganda kuandaa fainali hizo za mwaka 2027 ambazo kwa mara ya kwanza zitafanyika Afrika Mashariki.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mati Super Brands Limited, David Mulokozi (kushoto), akipeana mkono na Mkurugenzi Mkuu wa Timu ya Fountain Gate FC, Japheth Makau, baada ya kutia saini mkataba wa udhamini wa mwaka mmoja wa timu hiyo jana. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Meneja aonya watovu wa nidhamu Simba, ikizindua jezi mpya mbugani

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Simba, umetangaza kumrejesha Patrick Rweyemamu kwenye nafasi ya Meneja wa timu hiyo, huku mwenyewe akisema amerejea kusimamia nidhamu ndani ya timu hiyo.

Rweyemamu aliwahi kushika nafasi hiyo ndani ya Simba kabla ya msimu uliopita kupelekwa kuwa kiongozi kwenye soka la vijana ndani ya Simba.

Rweyemamu ameteuliwa kuchukua nafasi ya aliyekuwa meneja wa timu hiyo, Mkenya Mikael Igendia.

Akizungumza akiwa Ismailia nchini Misri ambako alikwenda baada ya uteuzi, meneja huyo alisema kuna baadhi ya wachezaji huwa na dharau na mameneja kutokana na mishahara yao mikubwa, lakini yeye hufanya kila njia ili kurekebisha mambo.

„Mpira una vitu viwili au vitatu, kocha lazima aandaliwe mazingira rafiki ambayo ni nidhamu kwa wachezaji, kuna idara ya kitabibu, ukishaunganisha hivi vitu viwili ndiyo unakuwa umemrahisishia kocha kazi.

"Daktari atamwandaa mchezaji kimwili na kiakili, sisi mameneja nao lazima tumwandalie mazingira rafiki yaani kambi na nidhamu, bila hivyo huwezi kufanikisha kile ambacho unakitaka, vinginevyo kocha hawezi kupata kitu bora.

Nikisema nidhamu inajumuisha vitu vingi, kulala, kunywa, kula, starehe, mazoezi kwa hiyo inahitaji lazima Meneja uwe na Mamlaka, uwe na uamuzi mgumu unaoeleweka na usiopinda," alisema Rweyemamu.

Alisema kuna baadhi ya wachezaji ambao wanalipwa pesa nyingi lakini baadhi yao wanatumia hilo kudharau viongozi wao lakini kwake ni tofauti kwa kuwa atasimimamia nidhamu kwa kila mchezaji.

Wakati huo huo, klabu hiyo jana imezindua jezi zake za msimu ujao kwenye Hifadhi ya Wanyamapori mkoani Morogoro.

Viongozi wa klabu hiyo, wakiongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Imani Kajula, walionyesha jezi tatu za rangi nyekundu, nyeupe na bluu ambazo timu yao itazivaa kwenye mashindano mbalimbali pamoja na kuuzwa kwa mashabiki wake.

Jezi hizo zimezinduliwa wiki chache kabla ya kufanyika kwa tamasha la klabu hiyo maarufu ‚Simba Day' ambalo litafanyika Agosti 3 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# Meneja amkana Kibu Denis

INATOKA UK. 24

mwaliko kutoka Norway ambapo kuna timu inayoshiriki Ligi Kuu nchini humo inamhitaji.

„Ninafahamu Kibu yupo Norway alipata mwaliko huo kutoka kwenye timu moja inayoshiriki Ligi Kuu nchini humo, masuala mengine siwezi kuyazungumzia zaidi ya hayo," alisema meneja huyo.

Alisema sakata hilo limeanza baada ya mchezaji huyo kwenda mapumzikoni nchini Marekani.

Alisema yeye kama meneja wa mchezaji huyo anamtaka kukaa meza moja na uongozi wa Simba kama anataka kujiunga na timu hiyo ya Norway.

"Kibu anapaswa kufahamu, hakuna namna anaweza kuikwepa Simba kwani ana mkataba nao kama kuna jambo lolote ni vizuri kukaa mezani azungumze na viongozi wake kusudi jambo hili lifikie kikomo kabla timu haijarudi Dar es Salaam kutoka Misri," alisema.

Klabu ya Simba ilimwongezea mkataba wa miaka miwili nyota huyo ambao utafikia mwisho mwaka 2026 huku ikiwa imemlipa stahiki zake zote.

Katika taarifa ya Simba iliyotoka jana, imesema itamchukulia hatua za kinidhamu mchezaji huyo kwa utoro wake licha ya kutakiwa kuripoti kwenye kambi ya timu hiyo.

Kikosi cha Simba ambacho kipo Misri kwa zaidi ya wiki tatu sasa, kinatarajiwa kurejea nchini siku chache kabla ya kilele cha tamasha la ‚Simba Day' litakalofanyika Agosti 3 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa

# Dube afungua akaunti ya mabao Yanga

INATOKA UK. 24

Yanga nusura iandike bao dakika ya 25, kama mpira wa kichwa uliopigwa na Clement Mzize usingekwenda nje kidogo ya lango la wapinzani wao. Mzize alikuwa ameruka juu kuunganisha kwa kichwa, mpira wa krosi iliopigwa na Mudathir Yahaya.

Ilikuwa ni dakika ya 37, wakati Qobolwakhe Sibande alipokosa bao la wazi baada ya kubaki na kipa Khomein, lakini mpira ulitoka nje kidogo ya lango.

Kipindi cha pili Yanga iliingia kwa nguvu ikiwa na mastaa wake wote na kufanikiwa kupata bao hilo lililodumu hadi mwisho wa mchezo.

Hata hivyo TS Galaxy itabidi ijilaumu yenyewe kwani ilikosa mkwaju wa penalti kupitia kwa mchezaji wake, Siphesihle Maduna dakika ya 68 baada ya Duke kuunawa mpira ndani ya eneo la hatari.

# Michezo

Nipashe Alhamisi Julai 25, 2024


## Arsenal kumbakiza Smith Rowe

UKURASA 21





Wanamitindo wakionesha mwonekano wa jezi mpya za klabu ya Simba zilizozinduliwa jana kwenye Hifadhi ya Taifa Mikumi, Morogoro. **PICHA: MTANDAO WA SIMBA**

# Meneja amkana Kibu Denis

●●● Asema Simba walimlipa pesa zote na kusaini mkataba wa miaka miwili, ashangaa kwa nini...

**Faustine Feliciane na Shufaa Lyimo**

SIKU moja baada ya uongozi wa Simba kutoa taarifa kwa umma juu ya utoro wa mchezaji wao, Kibu Denis, Meneja wa mchezaji huyo, Carlos Silyvester, ameibuka na kumkana mchezaji huyo kutokana na kile alichokifanya.

Akizungumza jana kwa njia ya simu, Carlos, amesema kuwa hafahamu mchezaji wake kwa nini ameshindwa kuungana na timu huku akiwa amelipwa pesa zake zote za usajili na kusaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia timu hiyo.

Alisema amesikitishwa na kitendo cha mchezaji wake huyo kuonyesha utovu wa nidhamu kwa waajiri wake hao.

"Kwa hilo la utovu wa nidhamu siwezi kuiingilia maamuzi yatakayofanywa na Klabu ya Simba, binafsi sipendi kuona mchezaji wangu anakuwa hana nidhamu kwa viongozi wake," alisema Silyvester.

Meneja huyo aliweka wazi kuwa anachokifahamu mchezaji wake huyo alipata

INAENDELEA UK. 23

## Dube afungua akaunti ya mabao Yanga

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI mpya wa Yanga, Prince Dube, jana alifungua akaunti ya mabao katika timu hiyo alipopachika bao pekee katika mechi ya kuwania Kombe la 'Mpumalanga' dhidi ya TS Galaxy kwenye Uwanja wa Kanyamanzane, Afrika Kusini.

Akiwa ameingia kipindi cha pili, alitumia dakika 10 tu kupachika mpira nyavuni na kuipatia Yanga ushindi wa bao 1-0 ukiwa ushindi wa kwanza wa timu hiyo tangu itue Afrika Kusini kwa ajili ya michezo ya kimataifa ya michuano hiyo maalum ikiwa ni sehemu ya maandalizi yao kuelekea msimu mpya.

Dube, akiwa wingi ya kushoto, aliukimbilia mpira mrefu wa chini chini uliopigwa toka nyuma na kumuhadaa beki wa kulia wa timu hiyo, Nkosikhona Radebe, kabla ya kuujaza mpira wavuni kwa mguu wa kushoto.

Mechi hiyo ilionekana kuchangamka kipindi cha pili hasa baada ya Yanga kuingiza wachezaji wake tegemeo, Stephane Aziz Ki, Maxi Nzengeli, Khalid Aucho na nyota wapya Duke Abuya na Clatous Chama.

Mechi ilianza taratibu na kwa kiasi kikubwa kipindi chote cha kwanza haikuwa ya kuvutia, na huenda ni kwa sababu ya Yanga kutumia wachezaji wengi ambao hawawatumii sana kwenye michezo yake muhimu.

Dakika ya 19, Aboutwalim Mshery alilazimika kufanya kazi ya ziada alipotoka langoni ili kutompa nafasi Siphesihle Maduna kuyaona mapana ya goli, na akafanikiwa kwani shuti la mchezaji huyo liliishia mikononi mwake.

Hata hivyo, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi kama alivyoahidi kuwachezesha karibuni wachezaji wake wote, alilazimika kumfanyia mabadiliko kipa huyo dakika ya 33 na nafasi yake ikatwaliwa na Khomein Aboubakar ambaye amesajiliwa msimu huu akitokea Singida Black Stars na hata yeye pia dakika ya 61 akatoka na kumpisha Diarra.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >